CHUO CHA BIBLIA

VITABU VYA
MANABII WADOGO
HOSEA, YOELI, AMOSI, OBADIA, YONA, MIKA, NAHUMU, HABAKUKI, SEFANIA, HAGAI, ZEKARIA NA MALAKI

KITABU CHA TISA

Manabii Wadogo: Fafanusi

Tunaanza kuchunguza manabii wa mwisho kumi na wawili, ambao wanatajwa kama Manabii Wadogo. Kutajwa huku kunamaanisha kwamba vitabu vyao ni vidogo au vifupi kuliko vya manabii wakuu ambavyo tayari tumechunguza. Kwa kuwa hawa manabii kumi na wawili waliandika hapo baadaye katika historia ya Waebrania, mara kwa mara vilitengwa na kutajwa kama manabii wa baadaye. Waandishi wa kale waliviweka katika sehemu iliyotengwa, iitwayo, 'Kumi Na Mbili' kwa kuwa vimethaminiwa sana na hawakutaka kupoviteza.

Vitabu kumi na viwili vya ki historia vilio katika Agano la Kale vinadhihirisha utangulizi wa mazingira na hali iliyowapata manabii walioviandika katika mahubiri yao. Ili kudumisha usawa wako wa kihistoria, unahitaji kufanya ramani ambayo itaonyesha mahali manabii wanapopaswa kuorodheshwa katika historia ya Waebrania uliojifunza wakati tulipochambua vitabu vya historia katika Agano la Kale. Ingawa haya sio masomo makuu, bali masomo ya kutuimarisha katika ibada yetu, hebu nikukumbushe kuhusu kweli saba za historia ya Waebrania ambazo unahitaji kutilia maanani wakati unaposoma kuhusu hawa manabii:

1. **Ufalme**
2. **Ufalme uliogawanyika**

3. **Uvamizi wa Ashuru dhidi ya ufalme wa kaskazini.**
4. **Kuangamizwa kabisa kwa ufalme wa kaskazini**
5. **Uvamizi wa Babeli dhidi ya ufalme wa kusini.**
6. **Uvamizi wa Uajemi dhidi ya Babeli**
7. **Kurudi kutoka utumwa wa Babeli**

SURA YA KWANZA

Unabii Wa Hosea

Wengi wetu tunafahamu kwamba Mungu ni Upendo, je, lakini ni vitabu vingapi ambavyo umeona au kusoma kuhusu hoja hii ya upendo wa Mungu? Kitabu cha Hosea ni kitabu kilichovuviwa katika maktaba ya Kiungu kuhusu upendo Wake Mungu. Hosea alikuwa ameagizwa na Mungu kuwa nabii wa upendo Wake kwa makabila kumi ambayo yalifahamika kama Ufalme wa Kaskazini; ambayo kwa jina lingine, ni kama taifa la 'Israeli.' Aliuhubiri upendo wa Mungu wakati walipokuwa wameasi na kuabudu sanamu.

Ukweli wa kwanza tunaojifunza kutoka kwa nabii Isaya ni kwamba wakati Mungu anapotuita kufanya kazi kuu kwa ajili Yake, Yeye hututayarisha kwa ajili ya kazi hiyo kupitia ushuhuda wetu wa maisha. Mungu hutumia matukio ya kila siku tunayoishi kututayarisha kwa kila siku ambayo tutaishi na kumtumikia.

Fumbo Lenye Kusononesha

Mungu alimtambua Hosea kama yu tayari kuhubiri upendo Wake kwa watu wasio waaminifu kwa kuwa alikuwa ameoa kahaba kwa jina, 'Gomeri' **(1:2,3).** Hosea alimpenda sana na kumfanya mama wa watoto wake kana kwamba ndiye aliyekuwa mwanamke bora katika nchi hiyo. Baada ya miaka mingi, wakati Gomeri aliporudi kwa wapenzi wake, Mungu alimwongoza Hosea kumpokea tena katika nyumba yake, na kuzidi kumpenda **(3:1).** Haya yote yaliruhusiwa na Mungu ili kumtayarisha Hosea kuwahubiria Israeli upendo Wake usio na masharti pamoja na kupokelewa Naye.

Ingawa hawakustahili, Israeli walikuwa wamechaguliwa na Mungu kuwa watu Wake, jinsi Gomeri alivyochaguliwa na Hosea kuwa mke wake licha ya kuwa kahaba. Fumbo ni hadithi ambayo watu, pahali, na mambo yana maana zaidi kwa kutoa mwongozo kwetu katika tabia na kiroho. Ndoa ya Hosea ilikuwa fumbo lenye kusononesha kuhusu upendo wa Mungu usio na masharti kwa watu wa Israeli.

Mahubiri ya Hosea

Kuabudu sanamu kulikuwa jambo la kuendelea, dhambi isiopona ya watu wa ufalme wa kaskazini wakati Hosea alipohubiri ujumbe wake wenye ujasiri na uliohitajika kwa wakati huo. Zinaa ilikuwa imekidhiri kama sehemu kuu ya kuabudu sanamu. Hosea alikuwa mwenye usemi wazi bila kukificha cho chote wakati alipokuwa akihubiri.

Hapa tuna vifungu vilivyofanywa tafsiri nyepesi ambavyo vitakufahamisha mtindo wa mahubiri yake: *'Wanaume wa Israeli humaliza kunywa divai yao na kuwakimbilia makahaba. Upendo wao wa aibu ni mkuu kuliko ule walio nao kwa ajili ya heshima na stahi. . .divai, wanawake, na nyimbo zimewapokonya watu wangu akili zao. Kwa kuwa wao wakiuliza kipande cha mti kile wanachostahili kukitenda. . . . wao ni kama upinde ulio kombo ambao hauwezi kuilenga shabaha yake. Wao wameupanda upepo nao wataivuna tufani..... Israeli imeharibiwa; imelazwa miongoni mwa mataifa kama chungu kilichovunjika. Efraimu, utukufu wake utarukia mbali kama ndege.'*

Kwa kuwa wao walikuwa taifa lililochaguliwa na Mungu aliye wa Kweli, Hosea alichukulia kugeukia miungu wengine kama 'ukahaba wa kiroho' kinyume cha Mungu: *'Watu wangu wautafuta ushauri kutoka kwa sanamu za kuchongwa kwa miti na fimbo yake mpiga ramli yawashauri; kwa kuwa roho ya ukahaba imewapotosha, nao wamejifanya makahaba, kwa kumwacha Mungu wao.'*

'Hao wote ni wazinzi; wamekuwa kama tanuu iliyotiwa moto na mwokaji; huacha kuuchochea moto, tangu kuukanda unga hata umekwisha kutiwa chachu. Maana wamefanya moyo wao kuwa tayari kama tanuu. Efraimu ajichanganya na mataifa; Efraimu ni mkate usiogeuzwa.' Wakati Hosea alipohubiri: 'Kama walivyo watu, ndivyo atakavyokuwa kuhani', yeye alipaza sauti, 'Ninyi makuhani msimnyoshee mtu yeye yote kidole chenu. Mimi nakinyosha kidole changu kwenu ninyi.'

Kama matokeo ya kuabudu sanamu, walikuwa wachukuliwe mateka: *'Israeli imemezwa; sasa wamo miongoni mwa mataifa kama chombo kisichopendeza. Kwa maana wamekwea kwenda Ashuru, mfano wa punda wa mwituni aliye peke yake; Efarimu amejiri wapenzi.*' Utekaji nyara hadi uko Ashuru ulikuwa mbaya kwa ufalme wa kaskazini, kwa kuwa wao hawangelirudi tena katika nchi yao na kuwa wenyeji tena. Wale ambao walinusurika kiumiliki wa Ashuru wangetawanywa kote katika mataifa mengine ulimwenguni.

Upendo Wa Mungu Usio Na Masharti

Israeli wangeingia utumwani ingawa Mungu angewapenda, kuwarudisha na kuwaponya kiroho. *Nami nitakuposa uwe wangu milele; naam, nitakuposa kwa haki, na kwa hukumu, na kwa ufadhili, na kwa rehema. Nami nitakuposa kwa uaminifu; nawe utamjua BWANA **(2:19-20)**.'* Kurejeshwa huko kwa kiroho kwa Israeli ambako baadhi ya manabii walikuwa wamehubiri, bado hakujatimizwa. Itatubidi kungojea siku za mwisho ili kushuhudia kutimizwa kwa unabii huu.

Kwa ufasaha mwingi, Hosea aliuhubiri upendo wa Mungu: *Kwa kuwa mimi sizitaki dhabihu zenu, mimi nautaka upendo wenu ninyi; mimi sizitaki sadaka zenu, Mimi nawataka ninyi mnijue Mimi.' Hili kuifanya mioyo ya iwe sawa na Mungu, Hosea alihubiri sawa na vile Yeremia alivyohubiri: 'Jipandieni katika haki, vuneni kwa fadhili; uchimbueni udongo wa mashamba yenu; kwa maana wakati umewadia wa kumtafuta Bwana, hata atakapokuja na kuwanyeshea haki. Basi, mrudie Mungu wako; shika fadhili na hukumu; ukamngojee Mungu wako daima* **(10:12; 12:6).**'

Matumizi Ya Kiinjili Na Kibinafsi

Ingawa ni lazima tungojee kutimizwa kwa kurejeshwa kiroho kwa Israeli, sio lazima tungojee kumrudia Mungu wetu wa upendo katika kiroho. Kifungu kinachofahamika sana katika

kitabu cha Hosea ni njia bora ya kumalizia muhtasari wa ujumbe huu mfupi wa matangazo ulioyasikia kuhusu nabii Hosea:

'Njoni, tumrudie Bwana; maana yeye amerarua, na yeye atatuponya; yeye amepiga, na yeye atatufunga jeraha zetu. Baada ya siku mbili atatufufua; siku ya tatu atatuinua, nasi tutaishi mbele zake. Nasi na tujue, naam, tukaendelee kumjua Bwana; kutokea kwake ni yakini kama asubuhi, naye atatujilia kama mvua, kama mvua ya vuli iinyweshayo nchi **(Hosea 6:1-3).'**

SURA YA PILI

Unabii Wa Yoeli

Yoeli ndiye nabii wa pili kati ya manabii wadogo kumi na wawili. Ujumbe wa nabii Yoeli unajumuishwa katika msemo ambao yeye na baadhi ya manabii wadogo wanatumia: 'Siku ya Bwana.' Yoeli analiita tauni kuu ya nzige waliovamia ufalme wa kusini, 'Siku ya Bwana.' Anapoelezea tauni hiyo kama 'Siku ya Bwana,' pia, analinganisha uvamizi huu wa nzige na utekaji nyara unaokaribia kutoka Babeli. Kama manabii wale wakuu, anachanganya unabii wake kuhusu utekaji nyara kutoka Babeli na unabii kuhusu mjio wa pili wa Kristo.

Wengi wanamfahamu Yoeli kwa sababu ya unabii wake wa ajabu kuhusu Siku Ya Pentekoste. Wale waliokuwepo wakati wa kuzaliwa kwa Kanisa waliuliza swali hili, *'Jambo hili maana yake ni nini?'* Petro alianzisha ujumbe wake kuhusu Siku ya Pentekoste kwa kuwaambia, *'Hili ni lile ambalo lilisemwa naye Nabii Yoeli* **(Matendo 2:12,16).'** Yoeli alihubiri kuhusu Siku ya Bwana kwangu na kwako kwamba kuna wakati uliopita, wakati huu, na wakati ujao katika maisha yetu.

Tauni Au Baa La Nzige

Kitabu cha Yoeli kinaanza kwa kueleza kuhusu baa la nzige ambao walikuwa wameuvamia ufalme wa kusini. Yoeli alihubiri: Y*aliyosazwa na tunutu yameliwa na nzige; na yaliyosazwa na nzige yameliwa na parare; na yaliyosazwa na parare yameliwa na madumadu* **(1:4)**.' Baa hili la nzige ilitanda juu ya nchi ile na kuharibu mimea yote na kuiacha ukiwa baada ya uharibifu.

Wakati Yoeli anapolinganisha baa hili la nzige na 'Siku ya Bwana **(1:15),** alikuwa akiifanya Siku ya Bwana kuwa tukio la siku hiyo. Je! Nia ya Yoeli wakati alipofananisha Siku ya Bwana katika njia hii ilikuwa ni gani? Wakati aliposhuhudia uharibifu kutokana na baa lile la nzige na kusema kwamba lilitokana na Bwana, alikuwa akisema kwamba Mungu angali mkuu katika dhiki na taabu zetu. Naye anakubaliana na kundi lote la waandishi wa Biblia ambao wametaja kwamba huenda Mungu ndiye chanzo cha dhiki na misiba yetu pamoja na fanaka. Kwa kuwa yamkini baa lile la nzige liliwafanya watu kufikiria kwamba Mungu alikuwa amewatupilia mbali, Yoeli alitangaza kwamba Mungu alikuwepo hata siku ile, maanake hata siku ya msiba inaweza kuwa 'Siku ya Bwana' kwa wenye kumpenda na walioitwa kulingana na kusudi Lake. **(Warumi 8:28).**

Uvamizi Wa Babeli

Kundi la nzige hutenda kazi kama jeshi, wao huharibu cho chote kilicho karibu . Yoeli alitumia uharibifu wa 'jeshi' la nzige ili kushika sikio la watu wa Yuda na kuwatayarisha kwa unabii wake wa uharibifu utakaowajia kutoka kwa majeshi ya Babeli. Yoeli aliandika hivi: *'Hupiga mbio kama mashujaa; huupanda ukuta kama watu wa vita; nao huendelea mbele kila mmoja katika njia zake, wala hapotoshi safu yake. Huurikia mji; hupiga mbio juu ya ukuta; hupanda na kuingia ndani ya nyumba; huingia madirishani kama aingiavyo mwivi* **(2:7, 9).'**

Siku Ya Pentekoste

Baada ya Yoeli kutangaza kundi la nzige kuwa Siku ya Bwana wakati huo, na pia kuhusu uvamizi kutoka Babeli kama Siku ya Bwana hapo baadaye, kisha, alianza kuizungumzia siku nyingine ya Bwana-Siku ya Pentekoste. Akishiriki maneno ya Mungu ya unabii, Yoeli aliandika hivi: *'Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono* **(Yoeli 2:28).'**

Unabii huu sehumu yake ilitimizwa katika siku ya Pentekoste **(Matendo 2:1-4).** Tunasoma kwamba Roho Mtakatifu alishuka juu ya wale waliokuwa wamekutanika pamoja Siku ya Pentekoste. Wakati watu walipoona ndimi za moto zikikaa juu ya vichwa vya mitume, na kuwasikia wakizinena kwa lugha ambazo zilifahamika tu na watu waliokuwa wakizizungumza, pamoja na kusikia 'sauti ya upepo uvumao,' wao walimwuliza Petro, *'maana yake nini haya?' Naye Petro akajibu, 'jambo hili ni lile lililonenwa kwa kimnywa cha nabii Yoeli* **(Matendo 2:16)**.'

Kuridi Kwa Yesu Kristo

Tambua kwamba kupitia unabii wa Yoeli wa Pentekoste, Mungu anatufahamisha jambo kuhusu Siku ya Bwana iliopo katika siku za baadaye ambayo haikutokea siku hiyo.

'Nami nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu na katika dunia, damu, na moto, na minara ya moshi. Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo. Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliitia jina la Bwana ataponywa; kwa kuwa katika mlima Sayuni na katika Yerusalemu watakuwako watu watakaookoka, kama Bwana alivyosema; na katika mabaki, hao awaitao Bwana **(2:30-32).**

Yoeli, kwa ufasaha mkuu alitabiri Siku ya Pentekoste. Ukisoma unabii wake kuhusu Pentekoste kwa makini, utaona kuwa alikuwa akitabiri matukio ambayo hayakutokea Siku ya Pentekoste, bali yatatimika katika mjio wa pili wa Yesu Kristo.

Kama ilivyokuwa na manabii wote, wakati unabii wa Yoeli wa matukio kama uvamizi wa Babeli au pentekoste ulipotimika jinsi ilivyoandikwa, tunaweza kusisimuka kuhusu ukamilifu wa unabii kuhusu kuja kwa pili kwa Kristo.

Petro aliita Siku ya Bwana ya hapo baadaye kama 'Siku Kuu na ya Kutisha ya Bwana.' Wakati Petro anaandika kuhusu siku hii, anatilia mkazo tukio moja kati ya matukio mengi ambayo ni sehemu ya kuja kwa pili kwa Kristo. Kulingana na Petro, wakati siku hii itakapowadia, *'Mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea* **(2 Petro 3:10).'**

Matumizi Ya Kibinafsi

Bali na Yoeli kuhubiri siku ya leo ya Bwana na ya usoni, pia alituhimiza kama watu wa Mungu kuwashauri watoto wetu, kizazi cha usoni kuhusu siku ya Bwana **(Yoeli 1:2-3).**

Anatushauri kutambua kwamba kila siku ipitayo, na iliyopo wakati huu na ya usoni inahitaji kutambuka kama Siku ya Bwana. Wakati tukumbukapo jinsi Mungu ametenda maishani mwetu kwa wema wetu, pia tunahitaji kuwa na ujasiri huo katika mambo na mazingira yetu ya hapo baadaye **(Warumi 8:28).**

Mbona Mungu anataka sisi tufahamu kuhusu Siku kuu ya kuogofya ya Bwana? Ili tupate kufikiria kuhusu jinsi ambavyo twahitajika kuwa, hebu sikiza matumizi ya Petro ya kibinafsi wakati anatuambia kuhusu Siku ya Bwana ya usoni: *'Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake. Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu* **(2 Petro 3:14-15a)** Tunapotazamia kuja kwa Siku ya Bwana, Yoeli na manabii wengine wanafanya matumizi sawa na hayo ya Petro ambayo anawapa wafuasi wa Kristo changa moto.

SURA YA TATU

Unabii Wa Amosi

Amosi alikuwa mchungaji wa kondoo na mtunzi wa mikuyu aliyeishi katika mji mdogo wa Tekoa, takribani maili kumi na mawili kusini mwa mji wa Yerusalemu. Mungu alimwita kutoka ufalme wa kusini kutabiri kinyume cha ufalme huo, miaka hamsini kabla ya uvamizi na utekaji nyara kutoka kwa wana wa Ashuru. Tunajulishwa kwamba Amosi alihudumu enzi ya utawala wa mfalme Uzia katika ufalme wa kusini ambayo chini chake, milki ya Yuda ilinawiri kijeshi na kiuchumi. Wao waliamini kwamba hakuna adui alikuwa kichochea mashambulizi dhidi yao au kuhatarisha maisha yao. Lakini unabii wa Amosi ulizungumzia kinyume cha kunawiri kwa taifa la Yuda, umoja na la Israeli.

Hukumu Ya Mungu Yaja

Amosi alianza unabii wake kwa kunena maneno ambayo raia wa ufalme wa kaskazini walitaka kusikia - Yeye aliwaambia kwamba Mungu angewahukumu maadui wao **(1:3-2:3).** Jinsi alivyokuwa akitaja majina ya mataifa yaliokuwa maadui pamoja na hukumu itakayowajia, wale waliosikiliza mahubiri yake walifurahishwa na ujumbe wake - wao wangependa kusikia jinsi Mungu angewaadhibu wale walio wachukia. Lakini wakati Amosi alipopata sikio lao, aliwapasha habari mbaya: Yuda na Israeli pia wangehukumiwa **(2:4-8).** Aliilaumu Yuda kwa kuikataa sheria ya Bwana na kutotii amri za Mungu, ilhali Israeli dhidi ya tamaa na kutokuwa na haki miongoni mwa jamii, usherati pamoja na kulikashfu jina la Bwana.

Amosi aliendelea na unabii wake kinyume cha Israeli kwa kutabiri kuhusu uvamizi kutoka Ashuru. *'Naye apigaye mbio atapotewa na kimbilio; Wala aliye hodari hataongeza nguzu zake; Wala shujaa hatajiokoa nafsi yake; Wala apindaye upinde hatasimama; Wala aliye mwepesi wa mgiuu hataokoka; Wala apandaye farasi hatajiokoa nafsi yake; Naye mwenye moyo mkuu miongoni mwa mashujaa atakimbia uchi siku ile, asema Bwana* **(Amosi 2:14-16).'**

Ufalme wa kaskazini ungepuuzia ujumbe huu kwa kuwa wao walikuwa wakiishi nyakati za kunawiri na fanaka na majeshi ya ufalme huo yalikuwa na ushupavu ambao Amosi aliutaja katika mahubiri yake. Lakini, katika kipindi cha miaka hamsini ufalme huo wa kaskazini, yaani Israeli ulishindwa na watu wote wakachukuliwa mateka na majeshi ya Ashuru.

Mungu alijaribu kuzuia uvamizi huo kutoka kwa Ashuru kwa kuwapa fursa Israeli kutubu dhambi zao **(4:6-13).** Alizuia mvua isinyeshe juu ya nchi yao, akawapiga kwa ukavu na konga, wingi wa bustani zao na mashamba ya mizabibu na miti ikaliwa na tunutu, lakini hata hivyo, jinsi Mungu alivyowaambia kupitia nabii huyu, 'Ninyi hamkunirudia mimi **(4;8, 9, 10, 11).'** Kwa kuwa Israeli hawakutilia maanani mwito wake Mungu kutubu, Amosi alitabiri juu ya hukumu ya Mungu, na kwamba hukumu ile ingekuwa haina mwisho - Israeli hawangeweza kurudi katika nchi yao kutoka utumwani huko Ashuru.

Amosi alitabiri hukumu ya Mungu kwa kuhubiri maono matano ambayo Mungu alimpa. Hukumu ambazo zinaelezwa katika maono ya kwanza mawili ambayo yalionyesha baa la nzige na moto ulao ziliondolewa mbali wakati Amosi alipomlilia Mungu kwa rehema zake **(7:1-6).** Maono ya tatu, yalikuwa kuhusu timazi ambayo kazi yake ni kupima wima wa wa ukuta, yalionyesha sababu ya Mungu kuwakasirikia watu wake kwa kuwa wao hawakuwa 'wima', katika maisha yao kulingana na Amri Zake, ila wao walikuwa watu 'kombo' waliokataa sheria Yake na watakaoipokea hukumu.

Maono yale ya nne, yalikuwa kuhusu kikapu cha matunda yaliyokuwa yameiva sana ambayo yalionyesha kwamba hukumu ilikuwa imechelewa sana ambayo Mungu alitabiri kinyume chake katika maono ya tano, pale aliposimama mbele ya madhabahu na kulia, '*Vipige vichwa vya nguzo, hata vizingiti vitikisike; vivunje vipande vipande juu ya kichwa cha kila mmoja wao; nami nitamwua mtu wa mwisho wao kwa upanga; hapana hata mmoja wao; atakayekimbia, wala hataokoka hata mmoja wao* **(Amosi 9:1)**.' Katika maono haya, Mungu alionyesha kwamba hukumu Yake juu ya Israeli ilikuwa ya mwisho. Hakuna hata mmoja ambaye angetoroka, na au angeliepuka. Hata hivyo, hukumu yake Mungu ilikaribia.

Fursa Ya Kiroho Huongeza Kuwajibika

Amosi hakubagua Yuda au Israeli kutokana na hukumu ya Mungu juu ya mataifa. Badala yake, aliwaambia kwamba hukumu yao ingekuwa kali sana kuliko ya mataifa yale mengine yasiomjua Mungu. Dhambi zao zilikuwa na madhara kwa kuwa wao tayari walikuwa na fursa ya kiroho kulifahamu Neno Lake Mungu. Hata hivyo, wao hawakuishi kulingana na sheria na kanuni za Mungu. Kulingana na Amosi, kuwajibika kiroho kunalinganishwa na ule usawa wa fursa ya kiroho, nazo fursa zetu za kiroho zinafaa kutuwezesha kushawishika jinsi tunavyoishi maisha yetu.

Yale tunayotenda kuhusu kile tunachofahamu ni muhimu sana kuliko yale tunayofahamu. Tunahitaji kukumbushwa kwamba kuishi kulingana na ufahamu wetu ni muhimu zaidi kuliko kupokea elimu ya juu. Hali ikiwa kwamba walimwengu huamini kwamba elimu peke yake inatosha na ni utakatifu, ilhali nabii alihubiri kwamba ni kuitekeleza ile elimu, au hekima ambako humfanya mtu kuwa mwenye haki.

Ahadi Ya Kurejeshwa

Amosi kama manabii wale wengine, alihubiri juu kurudi kwa wana wa Israeli: '*Siku hiyo nitaiinua tena maskani ya Daudi iliyoanguka, na kuziba mahali palipobomoka; nami nitayainua magofu yake, na kuyajenga kama siku za kale; wapate kuyamiliki mabaki ya Edomu, na mataifa yote yaitwayo kwa jina langu, asema Bwana, afanya hayo* **(9:11-12)**.'

Unabii huu unazungumzia kuhusu kurejeshwa kiroho kwa Israeli kwake Mungu. Kurejeshwa huko kwa Israeli kiroho bado hakujafanyika. Tayari tumeshuhudia kurudi kwa Wayahudi ambao walikuwa wametawanyika kote ulimwenguni, na pia tumekuona kurejeshwa kisiasa kwa Israeli, lakini bado hatujashuhudia kurejeshwa kwao kiroho.

SURA YA NNE

Unabii Wa Obadia

'Tazama, nimekufanya mdogo kati ya maifa; umedharauliwa sana. Kiburi cha moyo wako kimekudanganya, Wewe ukaaye katika pango za majabali, Mwenye makao yako juu sana; Asemaye moyoni, Ni nani atakayenishusha mimi? Ujapopanda juu kama tai, Ijapokuwa kioto chako kimewekwa kati ya nyota, Nitakushusha kutoka huko; asema Bwana **(Obadia 1:2-4).'**

Hivi ndivyo kitabu cha Obadia kinavyoanza. Ni yapi ambayo Obadia alikuwa akizungumzia kuhusu watu wenye kiburi waliokuwa wakiishi katika pango za majabali, wakifikiri kwamba hakuna ye yote awezaye kuwashusha chini kutoka ndani ya viota vyao? Wengi husema kwamba kitabu hiki kinahitajika kuwaonya wale miongoni mwetu ambao huishi katika karne ya ishirini na moja kuhusu safari zetu za angani za kuwatafuta viumbe wengine wanaoishi katika sayari nyingine. Katika vizazi vilivyopita, mistari hii ilikuwa imetafsiriwa na kutumika kwa kweli kwamba Mungu hataki tuishi katika nyumba ndefu. Katika karne ya ishirini na moja, wengi hutafsiri mistari hii kumaanisha, 'ikiwa tutakuwa na kiburi kuhusu sayansi na usanifu mkuu, ufundi wa tekinolojia hivi kwamba tutajaribu kuishi katika sayari nyingine huko angani, Mungu atatunyenyekeza na kutushusha chini duniani tena.'

Obadia hakuwa akiandika kuhusu majumba marefu au anga za juu. Yeye alikuwa akiwaka kwa hasira takatifu, na kuyazungumzia katika hiki kitabu kifupi kati ya vitabu vyote vya manabii, kwa watu wenye uadui mkuu ambao walikuwa wametenda maovu makubwa kinyume cha wana wa Yuda wakati Yerusalemu ilipoanguka mikononi mwa Wababeli.

Njia Ya Edomu Imehukumiwa

Mungu alizungumza kupitia Obadia ili kulihukumu taifa la 'Edomu.' Taifa hili la watu waliokuwa wakiishi mahali ambapo unaweza kutembela siku ya leo panapojulikana kama 'Mji wa Waridi Nyekundu wa Petra' *(The Rose Red City of Petra)* katika nchi ya Yordani. Mitelemko ya ghafula ya majabali mekundu, yenye sehemu kubwa na wazi zilizochongwa ndani yake yamkini futi mia saba pande zote mbili huko unaposafiria juu ya farasi katika bonde kuu. Hizi nafasi kubwa zilikuwa wakati mmoja mji ambao ulikuwa nyumba kwa watu ambao Obadia anawaandikia.

Baada ya watu hawa kuvamia na kuharibu miji ya maadui wao, au misafara ya wafanya biashara matajiri; wao wangepanda juu kwa ngazi za kamba kisha kujificha katika mapango yaliokuwa katika miteremko ya makazi yao, mbali kabisa na maadui. Makao yao yaliyokuwa juu

kabisa yaliwafanya kufikiria kwamba walikuwa hawawezi kuangamizwa. Hii ndio sababu Obadia anaandika: *'Kiburi cha moyo wako kimekudanganya, wewe. . .Asemaye moyoni, Ni nani atakayenishusha mimi?* **(1:3).'**

Na je! kwa hakika hawa walikuwa watu wa aina gani? Hawa walikuwa kizazi cha Esau, nduguye Yakobo. Kitabu cha Mwanzo kilituambia kwamba Yakobo na Esau walikuwa mapacha, lakini walikuwa na thamani tofauti. Pia waliishi maisha yenye mitindo tofauti. Ingawa Yakobo alikuwa mkaidi na mtu wa kiroho, Esau alikuwa kafiri na wa kidunia, asiye wa kiroho, ambaye tunaweza kumtaja kama 'mtu wa mataifa.' Hii imeonyeshwa katika mafumbo ya kitabu cha Mwanzo wakati Esau aliunza haki yake ya kuzaliwa kwa Yakobo kwa bakuli ndogo ya mchuzi.

Wakati kizazi cha Yakobo kilipopokea jina (Israeli) kutoka kwake na kufanyika Wayahudi, naye Esau akawa mzazi wa watu wa Edomu, maadui wakuu wa Wayahudi. Watu wa Edomu walikuwa wenye chuki sana dhidi ya wana wa Israeli, na wakati wote walitafuta fursa ya kuungana na watu wengine katika harakati za kuwaangamiza Wayahudi.

Obadia aliandika unabii wake mfupi ili kutabiri juu ya kuanguka kwa Edomu, kuanguka ambako kulikuwa matokeo yaliyohusiana na chuki na mateso dhidi ya Wayahudi. Obadia alitangaza mashtaka manane dhidi ya Edomu. Na kwa mara nane, tunamsikia akisema: *'Ninyi hamngalifanya hivyo!'* (Watu wa Edomu kwa hakika walikuwa wameyafanya hayo yote).

'Ninyi hamngelifurahia msiba wa ndugu yenu, katika siku ya dhiki yake. Ninyi hamngefurahia siku ya uharibifu wake. Hamngejivunia siku yake ya kusetwa. Na hamngaliingia katika lango lake siku yake ya dhiki. Hamngelimdharau yeye siku yake ya uharibifu. Hamngeteka vitu vyake. Hamngesimama katika njia panda na kuwagawanya wakimbizi wake. Haungeleta mabaki yao siku ya msiba. Na kwa kuwa hamngelitenda hivyo, siku ya Bwana yawajia juu yenu.'

Wasomi wanaamini kwamba Obadia alikuwa akihukumu tabia ya Edomu wakati wa kuanguka kwa Yerusalemu chini ya utawala wa Zedekia. Mji wao uliteketezwa hadi majivu na watu wengi wa Yuda wakaangamizwa ilhali wengine wakachukuliwa mateka hadi Babeli. Watu wa Edomu walisaidia katika kuvizia na kuzingira mji wa Yerusalemu, na walihusika pia katika kupora na kuteka mji huo. Wakati Wayahudi walipokwepa janga hilo, watu wa Edomu waliwateka na kuwarudisha kwa Wababeli.

Obadia alitoka huku kuwaadhibu Edomu na kuungana na manabii wengine kuhubiri kuhusu Siku ya Bwana. Aliambia watu wa Edomu, kuwa *'Kama ulivyotenda, ndivyo utakavyotendewa* **(15).'** Wakati siku hiyo aliyotabiri itakapotimia, taifa la Edomu litaangamizwa na kukatiliwa mbali kabisa. Yeye alitabiri kuhusu chombo sahihi ambacho Mungu atatumia kuwaangamiza. Marafiki zao watawageuka, na hapatakuwa na cho chote kitakachobakia kwa taifa la Edomu: *'Na nyumba ya Yakobo itakuwa moto, na nyumba ya Yusufu itakuwa mwali wa moto na nyumba ya Esau itakuwa mabua makavu, nao watawaka kati yao, na kuwateketeza; wala hatasalia mtu awaye yote katika nyumba ya Esau;* kwa kuwa Bwana amesema hayo **(18).'** Unabii huu ulitimizwa jinsi ulivyotabiriwa. Taifa la Edomu lilitoweka katika kurasa la historia wakati lilipokataliwa mbali kabisa na Warumi mnamo mwaka wa 70 Baada ya kuzaliwa kwake Yesu Kristo.

Matumizi Ya Kiroho

Kote katika Biblia, mtu wa haki hulinganishwa na mtu asiye haki **(Zaburi 1, Mathayo 7:13-27; 1 Wakorintho 2:14-16).** Ikiwa tunafahamu hadithi ya Yakobo na Esau katika Kitabu cha Mwanzo, pamoja na maelezo ya mtume Paulo juu ya hadithi ile, sio vigumu kutambua kwamba unabii huu mfupi wa Obadia pia ni hadithi yenye mafumbo ya kulinganishwa kwa maisha ya mtu wa kiroho na asiye wa kiroho, mtu wa kawaida kwetu **(Mwanzo 25:29-34; 27; Warumi 9:10,11).** Maisha ya Yakobo ni mfano wa mtu wa kiroho kwa kuwa alimtafuta Mungu na thamani za kiroho pamoja na baraka Zake.

Pia tunajifunza katika kitabu cha Mwanzo kwamba wakati Yakobo 'alipigana mieleka' na Mungu, jina lake lilibadilishwa na kuwa Israeli: *'Akamwambia, jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda* **(Mwanzo 32:28).** Naye Esau kwa upande mwingine, ni picha ya mtu wa kawaida, asiye wa kiroho. Kwa kuuza haki yake ya kuzaliwa (urithi wake mwana wa kwanza), kwa bakuli ya mchuzi, Esau alidhihirisha kutokomaa kwake na uovu wa thamani zake. Hatupaswi kushangaa kupata thamani na mfumo wa maisha ya 'Esau' huleta 'Edomu' - taifa lenye ukatili na upinzani kwa watu wa kiroho, wenye thamani za kiroho, na makusudio ya Mungu.

Tunapokutana na Yakobo na Esau kwa mara ya kwanza, wao wanaishi pamoja katika tumbo la mama mzazi, Rebeka. Hadithi yenye mafumbo iliopo katika tukio hili ni kwamba Esau na Yakobo wamo katika ulimwengu huu wa sasa ndani ya kila mmoja wetu.

Paulo anaelezea watu hawa wawili vyema katika waraka wake kwa Wagalatia. Anaandika kwamba mwili na Roho zinapigana moja kwa mwingine kwa kuwa ziko kinyume cha yule mwingine. Wakati Paulo alitumia neno 'mwili,' alimaanisha, 'asili ya binadamu ambayo haina msaada wa Mungu.' Roho Mtakatifu hutupa uwezo wa kiroho na kuwa kama Yakobo, lakini wakati Roho Mtakatifu anapokuja kuishi katika maisha yetu, mwili wetu, na asili ya kibinadamu, haziondolewi. Mtu aliye na juhudi la kutufanya kuwa watu wa kiroho ameongezwa katika miili yetu. Hii inatupatia uwezo huo wa wawili (Yakobo na Esau). Unabii wenye nguvu wa Obadia unatupatia changa moto na swali hili: Ni uwezo upi ambao sisi tutaupalilia?

SURA YA TANO

Unabii Wa Yona

Kitabu cha Yona kinatufunza juu ya nabii aliyeitwa na Mungu kuhubiri toba na wokovu kwa maadui zake. Yeye alifahamu mengi kuhusu asili ya Mungu kuwa ikiwa ataitikia mwito Wake, maadui zake wangeokolewa. Ni ufahamu wake kibinafsi kuhusu upendo wa Mungu usio na masharti ambao ulimfanya Yona kukataa kwenda Ninawi, na kwa sababu hakutaka kwenda huko, aliamua kwamba hataki kumwendea Mungu. Badala yake, alijaribu kutoroka mbali na Mungu na kupanda ndani ya merikebu ambayo bali na kuwa lilikuwa likisafiri upande ule

mwingine, pia lilikuwa likisafiri katika bandari ya mbali, jinsi mwanadamu wa siku zake angeweza kusafiri nje ya mji wa Ninawi **(1:3; 4:2,3).**

Mji wa Ninawi ulikuwa jiji kuu la maadui wa Wayahudi wa Kale. Ukatili wa watu wa Ashuru haukuwa na kifani katika ulimwengu wa wakati huyo. Yona au jamii zake walikuwa wahanga wa ukatili wao. Hivyo basi, alikuwa na sababu nzuri kuwachukia watu hao ambao waliishi katika mji huo wa Ninawi. Ili Kupata mtazamo wa kihistoria, hebu fikiria juu ya Mungu akimtuma Myahudi miaka ya 1940 kwenda *Berlin* Ujerumani, mahali kifo cha kila Myahudi ulimwenguni kilipangiwa, na kuhubiri hukumu ya Mungu juu ya mji huo ikiwa wao hawatatubu dhambi. Je! Yule Myahudi angekwepa wajibu kama huo?

Yona Haendi Kule Wala Haji (sura ya 1)

Manabii na waaminifu wa Agano la Kale walifuata mfumo fulani katika uhusiano wao na Mungu. Nilitaja mfumo huu wakati tulipotazama huduma ya nabii Isaya. Wao walikuwa na ujuzi wa maana wa kuja na kwenda kwa niaba ya Mungu. Hadithi ya Mungu kuhusu Yona ni kinyume cha mfumo huu.

Katika sura ya kwanza ya unabii huu mfupi wa Yona, tunasoma kwamba wakati Mungu alipomwagiza Yona kwenda Ninawi, alikataa kabisa na kudhihirisha kwamba aliamini hali mbili za kumjia na kwenda kwa niaba ya Mungu. Yona alifahamu kwamba alikuwa na ufahamu mkuu katika kumjia Mungu na ndio sababu alipokea mwito kwa kwenda huko Ninawi kwa niaba Yake. Kwa sababu hakunuia, wala kutaka kutenda hivyo, alitangaza kwamba hangeenda huko Ninawi kwa niaba ya Mungu, na kushikilia uamuzi huo.

Kwa sababu Yona alikuwa akijaribu kijificha mbali na Mungu wakati alipopanda Merikebu, alishuka hata pande za ndani kabisa na kulala usingizi mzito **(1:5).** Tunasoma kwamba Bwana alileta tufani kuu ambayo karibu iizamishe ile merikebu. Huku wale mabaharia wakiwa na hofu kuu na kuomba miungu wao, Yona alikuwa katika usingizi mzito, akijaribu kumkimbia Mungu wake. Yona alikuwa akijaribu kutoroka mbali na Ninawi, mbali na Mungu, na mbali na matatizo yake.

Wakati nahodha wa merikebu ile alipokumbana naye amelala wakati wa tufani kuu, Yona alikubali kwamba Mungu wake ndiye aliyesababisha bahari kuchafuka kwa kuwa amekasirishwa naye. Alikuwa ameituma tufani kuu maana alikuwa amemwagiza Yona kwenda huko Ninawi naye alikataa **(9-10).** Yona pia alimwambia yule nahodha kwamba njia ya pekee ya kuepuka balaa na hasira ya Mungu wake ni kumtupa nje ya merikebu hadi baharini, jambo ambalo walitenda mwishowe, ingawa kwa kulazimishwa **(15).** Punde tu ile tufani ikatulia na bahari ikaacha kuchafuka.

Kutulia kwa bahari kuliwafanya wale mabaharia kuamini. Hata wakati Yona alipokuwa akitoroka mbali na Mungu, mbali na yale ambayo Mungu alimtaka kutenda, Mungu alimtumia kuleta imani kwa wale mabaharia katika merikebu.. tunasoma, '*Ndipo wale watu wakamwogopa Bwana mno, wakamtolea Bwana sadaka, na kuweka nadhir*i **(1:16).**' Pia tunaendelea kusoma kwamba

Mungu alikuwa ametayarisha samaki mkubwa ili kumumeza Yona. Alikuwa tumboni mwa yule samaki mkuu kwa siku tatu. Yona hamwiti huyu samaki mkubwa nyagumi. Samaki huyu mkubwa alikuwa tendo la Mungu lisilo la kawaida, Alilotayarisha kwa ajili ya nabii huyu mwenye kuasi.

Yona Amjia Mungu(sura ya 2)

Kitabu cha Yona kinatufundisha kwamba ingawa kuna kweli kwamba Mungu hawezi kutulazimisha kutenda jambo fulani - Yeye hutuhusu kufanya uamuzi wa mapenzi yetu wenyewe kwa yale yaliyo mbele zetu - Yeye hutulalia kama ndovu katika mazingira hayo hadi tutakapofanya uamuzi kutenda mapenzi yake kwa ufahamu kwamba ndio jambo la kipekee lililo jema la kutenda. Unaweza kuandika kutoka upande mmoja hadi mwingine katika sura ya pili maneno haya mawili, 'Mimi nitafanya!'

Ilichukua siku tatu katika tumbo la yule samaki mkubwa kufanya Yona atubu kwa kutoroka mbali na mwito wa Mungu. Maana ya kutubu ni, 'kufikiria tena,' au 'kuwa na mabadiliko ya mawazo, nia, moyo, mapenzi na mwelekeo.' Umuhimu wa sura ya pili ni kwamba Yona alitubu akiwa ndani ya tumbo la yule samaki mkubwa. Yona aliomba akiwa ndani mwa tumbo la samaki yule. Alikumbuka kila andiko ambalo angewazia akiwa mahali hapo. Katika maombi yake, alikariri mistari ya Maandiko karibu sitini, kutoka kitabu cha Ayubu, Maombolezo, Samweli wa Kwanza, Yeremia, Wafalme wa kwanza na mistari mingi kutoka Zaburi. Hii inamaanisha mawazo yake yalikuwa yamejaa Maandiko, na pia aliimba Zaburi ambazo angekumbuka wakati alipokuwa ndani ya tumbo la yule samaki mkuu.

Jambo la muhimu kuhusu maombi haya ya Kibiblia ni toba yake. Yona alianza kwa kusema, 'mimi sitatenda hivyo,' hadi kusema mara tatu, 'Nitatenda hivyo.' *Alimwambia Mungu, 'mimi nitatazama tena kukabili Hekalu lako takatifu* ***(4).'*** *'Lakini mimi nitakutolea sadaka kwa sauti ya shukrani nitaziondoa nadhuiri zangu. Wokovu hutoka kwa Bwana* **(9).'** Kwa sababu ya toba ya Yona, Mungu *'akasema na yule samaki, naye akamtapika Yona Pwani.'*

Yona Aenda Kwa Niaba Ya Mungu (Sura ya 3)

Katika sura ya 3 tunasoma: *'Neno la Bwana likamjia Yona mara ya pili, kusema..* (**1).**;' Kutokana na tabia ya uvumilivu wa Mungu, Yona alisikia mwito kwa mara nyingine - mwito wake ambao ulibaki kuwa ule ule: '*Ondoka uende Ninawi, mji ule mkubwa, ukaihubiri habari nitakayokuamuru* **(2).**'

Mara hii, badala ya kukimbia mbali, Yona alitii mwito na kwenda hadi Ninawi. Aliuhubiri ujumbe wa Mungu wa hukumu kwa kutangaza: *'Baada ya siku arobaini Ninawi utaangamizwa!* **(4)**.' Mji wote - hata mfalme - walisadiki na kumwamini Mungu **(5, 6).** Kwa kuwa mji huo ulitubu, *'Mungu akaona matendo yao, ya kuwa wameiacha njia yao mbaya. Basi Mungu akalighairi neno lile baya, ambalo alisema atawatenda; asilitende* **(10).'** Mwishowe Yona aliposema kwamba 'nitatenda hivyo,' matokeo yalikuwa uinjilisti mkuu katika historia ya Mungu na mwanadamu.

Yona Haja Na Kwenda Kwa Niaba Ya Mungu (Sura ya 4)

Kina cha ujumbe wa Kitabu cha Yona kinapatikana katika sura ya mwisho pale tunaona jinsi Yona alivyohusika katika kughairi kwa Ninawi. Ingawa tungefikiri kama nabii wa Mungu, angekuwa mwenye furaha isiyo kifani, kwa kuwa mji mzima ulikuwa umetubu na kumgeukia

Mungu, badala yake alikasirika. Kwa hakika alikuwa mwenye hasira, kiasi kwamba ingekuwa bora kufa kuliko kushuhudia Mungu akiokoa umati wote wa Ninawi - hata kumwambia Mungu hayo! Badala ya kumsifu Mungu, Yona alimwambia: *'Ee, Bwana; sivyo hivyo nilivyosema, hapo nilipokuwa katika nchi yangu? Hii ndiyo sababu nalifanya haraka kukimbilia Tarshishi; kwa maana nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa rehema, nawe waghairi mabaya. Basi, sasa, Ee Bwana, nakuomba, uniondolee uhai wangu; maana ni afadhali nife mimi kuliko kuishi* ***(2,3).***' Kwa maelezo mengine, *'ingelikuwa bora nife kuliko kuona wewe ukiwaokoa watu hawa"*

Nabii Mwenye Chuki

Ni nini mbaya na Yona? Jibu kwa swali hilo ni kwamba, Yona alichukia watu wa Ninawi, na ilikuwa ni kupendelea kwake kulikomfanya kutoshukuru kwa muijiza huo uliotokea katika mji huo mkuu wa ufalme wa Ashuru. Upendeleo wake unadhihirishwa na kukiri hapo mwanzoni mwa sura ya nne, kwamba alitoroka mbali na Mungu, kwa kuwa alifahamu kwamba Mungu alikuwa mwenye upendo na angeokoa mji wa Ninawi ikiwa angelimtii na kuhubiri huko.

Ili kukumbana na hasira ya Yona, Mungu alimpa funzo la ishara. Hali Yona akisononeka kwa hasira, huku akimtupia Mungu maneno kwa kuwaokoa maadui zake, alijifanyia kibanda huko mashariki mwa mji juu ya mlima huko Ninawi. Kwa hakika, alikuwa angali akiamini kwamba, au alikuwa akitumainia kuwa Mungu angeangamiza mji huu muovu. Nalo jua lililokuwa kali lilimchoma Yona wakati Mungu alipolifanya mtango ukue juu yake, ili uwe kivule juu ya kichwa chake, na kumponya katika hali mbaya. Jambo ili lilimpendeza Yona sana. Lakini siku ya pili Mungu alimtuma buu na kutafuna ule mtango. Yule buu akakata mtango huo na Yona mara moja apandwa na hasira tena.

Mungu alimwambia Yona, *'wewe umehurumia mtango, ambao hukuufanyia kazi, wala kuuotesha; uliomea katika usiku mmoja,na kuangamia katika usiku mmoja; na mimi je! Hakunipasa kuuhurumia Ninawi, mji ule mkubwa; ambao ndani yake wamo watu zaidi ya mia na ishirini elfu, wasioweza kupambanua katika mkono wao wa kulia na mkono waa wa kushoto; tena wamo wanyama wa kufugwa wengi sana?* **(11)**.' Wasomi hukisia kwamba hawa ni watoto wa Ninawi ambao wangali hawajafikia umri unaofahamika kama wa kuwajibika. Ukweli hapa ni kwamba Mungu alikuwa akilipa changa moto thamani na kipao mbele cha nabii mwenye chuki.

Kikwazo Cha Shida

Unaweza kukumbuka kwamba katika ukaribio wangu kwa manabii, nilishiriki nawe kuwa moja ya kazi za nabii ni kuiondoa kikwazo cha shida zilizokuwa zikizuia kazi ya Mungu duniani. Katika kitabu cha Yona, kikwazo kilichokuwa kikikwaza muujiza wa kazi Mungu aliyonuia kutenda huko Ninawi kilikuwa ni chuki ya nabii Yona.

Jinsi tulivyojifunza naye Hosea, upendo wa Mungu hauna masharti na hautegemei kazi nzuri au mbaya kutoka kwa mwenye kupendwa. Ikiwa Mungu anawapenda watu naye nabii anawachukia, je! Mungu anawezaje kumtumia nabii kama huyo kuutangaza upendo Wake kwao?

Matumizi Ya Kibinfasi

Je! Unajitambua katika hadithi hii? Je Unakimbia mbali na mwito wa Mungu ambao ameweka juu ya maisha yako? Ni kitu gani ambacho ni lazima Mungu akitume ili kukufanya kukubali kumtii? Jifunze katika maisha ya Yona - nabii ambaye hakutaka kwenda Ninawi na ambaye hakutaka kumwendea Mungu - Kwamba Mungu hutumia mazingira ya maisha yetu ili kutuongoza katika mapenzi yake kwa ajili ya maisha yetu, licha ya kutotii kwetu kumfuata. Unaweza kutambua kwamba kitabu hiki kifupi cha unabii kimejaa maongozi ya Kiungu: Mungu hutuma tufani kuu, humtayarisha samaki mkubwa, hukata mtango na pia humtuma buu. Je! Unaona uongozi wa Mungu ukitenda kazi katika mazingira yako?

Eneo lenye uwezo mkuu katika kitabu hiki cha unabii imetiliwa mkazo wakati tunapotambua kwamba Yona aliandika kitabu hiki, ambacho kwa hakika kinamfanya kuonekana mpumbavu sana. Yona anaandika sura muhimu sana katika maisha na huduma yake kama nabii wa Mungu. Anatueleza na kwa njia ya kunyenyekea sana, jinsi alivyojifunza katika mji wa Ninawi kuhusu upendo wa Mungu ambao hauna masharti kwa wenye dhambi - na kuwa chuki kilikuwa katika moyo wake ambao ulikuwa kikwazo dhidi ya dhihirisho la upendo huo.

Yona alishiriki ungamo la kweli na la nabii mwenye kweli katika kitabu hiki ambacho kina jina lake. Kwa hakika, alikiri kwamba: ‘Mimi sikuwa upendo usio na masharti huko Ninawi, ila Mungu alikuwa upendo huo, naye alikuwa pamoja nami. Niligundua kwamba singewapenda watu waovu wa Ninawi, bali Mungu alitaka kuwapenda, naye alikuwa pamoja nami. Mimi sikuwapenda watu wa Ninawi, lakini Mungu aliwapenda kupitia mimi kwa kuwa Alikuwa pamoja nami.’

Je! Inawezekana kwamba Mungu anataka kuwapenda watu waovu wasiopendeka, na wenye dhambi zaidi yako, lakini chuki yako kwao inakwaza upendo na wakovu Wake? Je! Unaweza kujiona katika hali hii iliyo wazi na ya kweli ya kukiri kwa nabii huyu mwenye chuki mbaya?

SURA YA SITA

Unabii Wa Mika

Kitabu hiki kinanukuuu jumbe tatu za nabii Mika. Yeye alizaliwa mashambani katika vitongoji vya mji mkuu lakini alikuwa ameitwa na Mungu kuhubiri katika miji mikuu ya Samaria na Yerusalemu na kuzungumzia maneno Yake kwa viongozi wa kisiasa na wale wa kiroho wa miji hiyo ya Yuda na Israeli. Aliungana na manabii wengi kushtumu ufisadi wa tabia na kiroho wa watu wa Mungu juu ya viongozi wa kiroho na wale wa kisiasa katika falme zote mbili.

Mahubiri Ya Kwanza Ya Mika (1:3-5)

Mahubiri ya kwanza kati ya tatu ya Mika yalihubiriwa kwa watu wote wa dunia na kuwakaribisha kushuhudia ‘mapigo’ ya ufalme wa kaskazini na kusini yaani Israeli na Yuda. Kwa kuwa watu wa Mungu walikuwa wakichagua kutofuata njia zake, Yeye alikuwa akipanga adhabu ya baadaye: ‘*Basi Bwana asema hivi, Angalia, nakusudia jambo baya juu ya jamaa hii, ambalo hamtazitoa shingo zenu, wala hamtakwenda kwa kiburi; kwa maana ni wakati wa mbaya* **(2:3)**.’ Msitari

huu kwa hakika unazungumzia kuhusu uvamizi na utekaji kutoka kwa Babeli na Ashuru. Kupitia uvamizi na utekaji huo, Mungu angewaadhibu Yuda na Israeli, nayo adhabu hii itakuwa dhihirisho ya utakatifu Wake, kwa kutovumilia kwake uovu, na upendo kama Baba mwaminifu kwa watoto wake waasi.

Adhabu ya Mungu kwa watu Wake kwa ajili ya ibada ya sanamu, usherati pamoja na kufifia kwa kiroho ingeonyesha ulimwengu wote kwamba Mungu anahitaji kiwango cha juu cha utakatifu. Utukufu wa Mungu utafunuliwa kupitia kurejeshwa kwa watu wake, ambako Mika alihubiri hapo mwisho wa ujumbe wake wa kwanza: *'Hakika nitakukusanya, Ee Yakobo, nyote pia; Bila shaka nitawakusanya waliobaki wa Israeli* **(2:12).'**

Mahubiri Ya Pili Ya Mika (3:1-5:15)

Mahubiri ya pili yalizungumziwa katika daraja tatu za serekali: Makuhani, manabii, na viongozi wa kisiasa. Kazi kuu na ya msingi ya kuhani ilikuwa kufundisha, ilhali wajibu mkuu wa manabii ulikuwa kubashiri na kuwahimiza watu kuwa watiifu na wadhfa mkuu wa viongozi wa kisiasa ni kutilia mkazo udumishaji wa sheria za Mungu. Katika siku za Mika, shida na kikwazo kilichokwaza kazi ya Mungu kilikuwa ni daraja hizi za mfumo wa uongozi uliochaguliwa na Mungu ambazo ni fisadi.

Badala ya kufundisha na kuitekeleza sheria ya Mungu kwa watu, makuhani walichagua *'kufundisha ili wapate ijira' , au 'kufundisha kwa malipo* **(3:11).'** Walikuwa wakibadilisha mwito wa makuhani kuwa kama kazi ya malipo, na haja yao kuu ilikuwa fedha walizopata. Mika alifedheheshwa na tabia hii ya kufanya kazi ya makuhani kuwa biashara ambayo kufundisha kwao kwa ajili ya ijira kuliwafanya kuwa watenda kazi wa malipo yaliokuwa kafiri kwa Mungu.

Vivyo hivyo, manabii walipuuza mwito wa Mungu kuwa manabii kwa kuchagua *'kutabiri ili wapate fedha (1.'1).'* Bali na kuwa walibadilisha mwito wa nabii kuwa kazi ya ujira, pia na uchawi. Walikuwa wakihubiri ndoto zao tu, badala ya ufunuo wa unabii, pamoja na kutumia sifa zao kama manabii kujipatia faida. Walipolipwa fedha kidogo, wao walikuwa wakitabiri uovu pamoja na hukumu kwa watu, lakini wanapopokea fedha nyingi, wangetabiri mema katika maisha ya watu walio walipa.

Nao viongozi wa kisiasa walikuwa wafisadi na walichagua *'kuhukumu ili wapate rushwa* **(11).**' Kutegemea malipo waliopokea, viongozi hawa wa kisiasa wangefanya hukumu kwa kupendelea kulingana na yule aliyewalipa. Ufisadi wa viongozi wa kisiasa, umekuwapo na upo kote ulimwenguni hata siku ya leo.

Hoja kuu ya Mika ni, wakati makuhani wanapofunza kwa ajili ya ijara, watu huchanganyikiwa kwa kuwa hawajifunzi Neno la Mungu. Wakati manabii wanapofanya unabii kwa malipo, watu wa Mungu hawasikilizi Neno hilo. Wakati viongozi wa kisiasa wanapokuwa fisadi, watu hukata tamaa na kupoteza imani kwa serikali, pamoja na sheria na utangamano.

Mika anatilia mkazo kweli kwamba Mungu ndiye aliyewapa jukumu hilo, lakini serikali iliyochaguliwa na Mungu inaweza kutenda kazi tu ikiwa wale wanaowajibika kuifanya wanashiriki

na kuungana na Mungu kwa hali ya kiroho na serikali katika daraja hizi tatu. Ikiwa viongozi katika daraja hizi tatu ni wafisadi, makusudio ya Mungu kwa ajili ya serikali huvunjika. Kwa kuwa viongozi wa kiroho na kisiasa siku za Mika hawakuwa wameungana katika nia ya Mungu, yeye alikuwa akiwalaumu kwa kuvunjika kiroho na kudhoofika kwa maadili katika taifa.

Suluhisho La Mwisho La Mungu

Baada ya kuzungumzia kwa dhati kushindwa kwa serikali huko Yuda na Israeli, Mika aliuhubiri ujumbe wa tumaini kwa watu wa Mungu na mataifa yote ya ulimwengu kupitia unabii wa Kimasihi. Alitabiri kuja kwa Masihi, ambaye *'atasimama, na kulisha kundi lake kwa nguvu za Bwana, kwa enzi ya jina la Bwana, Mungu wake; nao watakaa; maana sasa atakuwa mkuu hata miisho ya dunia. Na mtu huyu atakuwa amani yetu (***5:4-5).'**

Mahali serikali ya binadamu iliposhindwa huko Yerusalemu na Samaria, mamlaka makuu ya Kristo hayangefaulu, naye atatileta amani kwa watu wake. Yeye atakuwa mfano bora wa nabii, kuhani na mfalme. Mwishoni mwa ujumbe wa pili, Mika alimdhihirisha Kristo kama kiongozi mkamilifu. Yeye atauleta ufalme mpya ambao hautakuwa na uharibifu wala ufisadi. Kwa sababu hii, wakati Kristo alipokuja duniani, wanafunzi wake walimhoji kuhusu wakati atakapouleta ufalme mkamilifu na usio na mwisho **(Matendo 1:6).**

Mahubiri Ya Tatu Ya Mika (Sura ya 6 na 7)

Katika mahubiri ya Mika ya tatu, anawasilisha kesi ya mahakama ya kifumbo kati ya Mungu na mwanadamu. Yeye anahubiri: *'Basi sasa, sikieni asemavyo Bwana; Simama, ujitetee mbele ya milima, na vilima navyo na visikie sauti yako. Sikieni, enyi milima, mateto ya Bwana, na ninyi, enyi misingi ya dunia iliyo imara; kwa maana Bwana ana mateto na watu wake, naye atahojiana na Israeli* **(6:1-2).'**

Vile Mika anapowasilisha shtaka lake Mungu dhidi ya Israeli, Mungu aikumbusha Israeli kuhusu wema wake kuwatoa huko Misri na kuwapa Musa, Haruni, pamoja na Miriamu ili kuwaakilisha **(4).**

Kwa kuwa watu wa Israeli hawakuitikia wema wa Mungu kwa kufuata miungu mingine na kutekeleza tamaa zao za kibinafsi, Mika aliwakilisha hali ya binadamu mbele ya hukumu ya Mungu: *'Nimkaribie Bwana na kitu gani, na kuinama mbele za Mungu aliye juu? Je! Nimkaribie na sadaka za kuteketezwa, na ndama za umri wa mwaka mmoja? Je! Bwana atapendezwa na elfu za kondoo waume, au na elfu kumi za mito ya mafuta? Je! Nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu?'*

Hukumu ya Mika kwa dhambi ya Israeli kutokana na uasi kwao kinyume na wema wa Mungu kuliwafanya Israeli wasiofaa kujitetea wenyewe. Mashtaka ya Mika ni kwamba hakuna sadaka ye yote ya dhambi iwezayo kwa utimilifu kuzifunika dhambi za Israeli.

Hali ambayo Mika aileta katika shtaka hili kuu katika *mahakama iliwatayarisha wasikilizaji wake kwa kumalizia ujumbe wake: 'Ee mwandadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!* **(8).'**

Baada ya kuwasilisha mashtaka yake dhidi ya watu na baadaye kuwauliza kile wawezacho kufanya hili waweze kumfurahisha Mungu, Mungu naye alimwonyesha Mika kwamba hakuna lo lote ambalo mwanadamu angetenda ili kuiondoa dhambi yake. Ni kupitia tu neema ambayo Mungu huitoa kwa moyo uliovunjika ndio mwanadamu aupokee msamaha wa dhambi zake.

Mika alimalizia ujumbe wake wa tatu kwa ufunuo mwingine wa unabii. Katika siku za mwisho, akawaambia Israeli: *'Mataifa wataona, na kuzitahayarikia nguvu zao zote; wataweka mikono yao juu ya vinywa vyao, masikio yao yatakuwa uziwi. . . watakuja kwa Bwana, Mungu wetu, kwa hofu, nao wataogopa kwa sababu yako* **(7:16, 17).'**

Hapa kwa mara nyingine tunaona kutimizwa kwa Kiongozi Masihi ambaye atatawala mataifa. Jinsi Mika anavyotabiri, Kiongozi huyu atakuwa mwenye rehema kwa watu wake waliochaguliwa: *'Hashiki hasira yake milele, kwa maana yeye hufurahia rehema. Atarejea na kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari. Wewe utamtimilizia Yakobo kweli yako, Ibrahimu rehema zako ulizowaapia baba zetu tangu siku za kale* **(7:18-20)**.;'

Mungu wa ujumbe wa Mika ni Mungu mwenye rehema na huruma, pamoja na upendo usio na masharti. Hii inamaanisha hatuwezi kushindania, au kupokea upendo wa Mungu kwa matendo yetu mema - Hii yawezekana tu kwa neema yake - na pia hatuwezi kupoteza upendo wa Mungu kwa matendo maovu.

Ukiuelewa vyema, ujumbe wa manabii ni wa tumaini na ambao misingi yake ni upendo na neema yake Mungu. Hata hivyo, upendo na neema ya Baba yetu aliye mbinguni zinasawazishwa na haki Yake - Haki ambayo inaweza kutoshelezwa na malipo yatokanayo na kifo cha Mwanawe wa pekee, ili tuweze kufurahia upendo na neema kamilifu ya Mungu milele.

SURA YA SABA

Unabii Wa Nahumu

Mtazamo Wa Kihistoria

Manabii ambao waliandika vitabu vya unabii katika Agano la Kale walinakili uvamizi wa miji minne: Yerusalemu, Samaria, Babeli na Ninawi. Yerusalemu na Samaria ndio ilikuwa miji mikuu ya falme za kusini na kaskazini yaani Yuda na Israeli, ilhali Babeli na Ninawi yalikuwa miji mikuu ya maadui zao. Jinsi tulivyoona, mahubiri ya Yona yalileta toba na wokovu huko Ninawi.

Unabii wa Nahumu unatangaza hukumu na kuangamizwa kabisa kwa mji huo. Nahumu anafuatia Yona kwa karibu miaka 120.

Hali kitabu cha Yona kinapozungumzia kuhusu toba ya mji mkuu wa maadui wakatili wa Israeli, miaka sitini baada ya toba ya Ninawi na mahubiri makuu ya Yona, Ashuru walivamia ufalme wa kaskazini wa Israeli na kutwaa mateka makabila yote kumi ya Israeli hadi kwao. Yamkini miaka sitini baada ya uvamizi na utekaji nyara wa Ashuru, Nahumu alitabiri kuja kwa hukumu na kuangamizwa kabisa kwa Ninawi. Unabii huu wenye kushangaza wake Nahumu ulitimilika baada ya miaka ishirini na mitatu tangu alipotabiri.

Ashuru waliwavamia na kuwafanya watumwa mataifa mengi ulimwenguni kwa ukatili mkuu sana. Ukatili wa upumbavu wao haukuwa na kifani katika historia ya ulimwengu wa wakati huo, na walivyozidi kuwa milki kuu, ulimwengu wote ulitia hofu na woga ukatili wao. Cha muhimu sana katika ufalme wa Ashuru kilikuwa mji wa Ninawi, ambao ulifahamika kama Mji mkuu ulimwenguni. Ni uharibifu wa huu mji mkuu duniani ambao ulitabiriwa na nabii Nahumu.

Nahumu Atangaza Kuangamizwa Kwa Ninawi (sura ya 1)

Sura ya kwanza ya kitabu cha Nahumu inatangaza kuanguka kwa Ninawi. Ingawa mito miwili ilikuwa imeulinda mji huo kutoka pande mbili, Nahumu alitabiri kuanguka kwake kutatokana na *'gharika ifurikayo atapakomesha kabisa mahali pake.'* Mito hii miwili ilitia nguvu mji ule kwa ulinzi wake wenye kuzungukia, lakini Nahumu alitabiri kwamba *'Bwana angekifanya kilicho shina la ulinzi kuinuka, na kugharikisha, na kupakomesha pahali pale* **(1:8).'**

Maana ya jina Nahumu ni 'faraja kamili,' nao ujumbe wake ulileta faraja katika ufalme wa kusini. Ashuru walikuwa tayari wameuteka nyara ufalme wa kaskazini, na wa kusini ulikuwa na hofu kwamba Ashuru wangewageukia na kuwateka pia. Baada ya Ashuru kuwavamia na kuteka watu wa ufalme wa kaskazini, kwa hakika waligeukia kusini na kuwateka. Wao walivamia na kuiteka miji arobaini na sita yenye kuta kubwa na kuchukua takribani watu laki mbili kuwa mateka wao.

Jinsi tulivyojifunza wakati tulipochambua unabii wa Isaya, wakati walipowasili katika malango ya Yerusalemu, kupitia huduma ya nabii mkuu, ufalme wa kaskazini ulinusurika maafa. Hata baada ya ushindi ule mmoja, ufalme wa kusini bado ulikuwa na hofu kutokana na uvamizi wa Ashuru. Unaweza kuona jinsi unabii wa Nahumu alivyokuwa akisema, *'Ijapokuwa wana nguvu zilizo timilifu, ijapokuwa ni wengi, hata hivyo watakatwa, naye atapita na kwenda zake*' na kuwapa faraja, amani, na tumaini katika nchi ile ya Yuda **(11).**

Nahumu Anaelezea Kuangamizwa Kwa Ninawi (sura ya 2)

Katika sura ya pili ya unabii wa Nahumu, anaeleza kuanguka kwa mji huo wazi wazi. Anaeleza rangi ya sare ya majeshi ya adui na jinsi jua litakavyo meta meta juu ya ngao zao **(3).** Kwa umakinifu mwingi, anaeleza mbio za magari ya vita na watu njiani ili kuepuka tukio hilo la uharibifu wa mji uliokuwa ukikataliwa mbali **(4).** Alitabiri jinsi wale wana jeshi walivyoondoka katika mji na nchi ile bila kuangalia nyuma **(8).** Katika maelezo ya Nahumu, malkia afuliwa na

kuchukuliwa hadi utumwani **(7).** Magoti yao yanagongana-gongana; na mioyo yao inayeyuka kwa hofu, viunoni mwote wana utungu, na nyuso zao wote zimekuwa nyeupe kwa hofu **(10).** Maelezo haya wazi yalionyesha ufalme wa kusini jinsi Mungu angewaletea amani na faraja katika nchi yao kupitia uharibifu wa mji mkuu wa maadui zao.

Nahumu Atetea Kuharibiwa Kwa Ninawi (sura ya 3)

Nahumu aliorodhesha baadhi ya sababu ya hasira yake Mungu dhidi ya Ninawi. Aliwashtaki kwa kuimwaga damu, kueneza uongo, kuangamiza miji mingine na kuhusika katika ukahaba. Wasomi wa historia ya kale wanaeleza kwamba Ashuru iliwahamisha watu iliowateka hadi nchi zingine hili kuvunja uzalendo wao, na kuwa walitenda mambo ya ukatili kinyume cha mateka wao. Waliwachuna ngozi na kuitoa wangali hai, na wakati wanapoteka mji, wangeangamiza nusu ya watu wake na kuweka magofu ya fuvu za vichwa kwenye malango ya mji huo hili kuwaogofya wale walionusirika maafa yale.

Kwa sababu kila taifa katika nchi ile lilikuwa limeteseka katika mikono ya wakatili wa Ashuru, na kama jibu kwa ukatili huo, Nahumu aliwaambia maneno haya ya Bwana: *‘ Tazama, mimi ni juu yako, asema Bwana wa majeshi; nami nitafuma marinda yako mbele ya uso wako; nami nitawaonyesha mataifa uchi wako na falme aibu yako* **(3:5)**.’ *‘Jeraha yako haipunguziki; jeraha yako ni nzito sana; wote wasikiao habari zako wapiga makofi juu yako* **(3:19)**.’ Kuanguka kwa Ninawi kutakuwa chanzo cha faraja kwa mataifa yote ambayo yalikuwa yakiishi kwa hofu kwa sababu ya ukatili wao.

Nahumu Aitetea Asili Ya Mungu

Kitabu kinatufunza kuhusu upendo na hasira ya Mungu. Kwa lugha ya Kiebrania, neno linalotumika kwa hasira ya Mungu linamaanisha ‘kuvuka.’ Wazo ni kwamba asili kamili ya Mungu ni upendo, lakini kuna wakati uovu na kukosa Uungu kwa watu kunapomlazimisha kutekeleza upande mwingine wa asili yake, ambao ni utakatifu na haki kamili. Katika hatua hiyo, Yeye, ‘huvuka’ katika hasira na hukumu yake kwa sababu, kwa uhakika mwishowe, uovu hauwezi kuchanganyika na utakatifu wa Mungu.

Kulikuwa na baba mmoja mwenye mapenzi, mpole ambaye iliwabidi askari kadhaa wa polisi kumkamata kwa nguvu wakati mtu, ambaye alikuwa amemnajisi na kumwua bintiye wa miaka saba, alipokuwa ameletwa katika kituo cha polisi. Ikiwa yule baba mzazi alikuwa na tabia ambayo ingelivuka kutoka upole hadi kupandwa na hasira, je! Inawezekana kutokee kuvuka kwa asili ya Mungu?

Hivyo basi tunaweza kufafanua hasira ya Mungu kama: ‘tabia ya kudumu, yenye kuambatana, iliyo thabiti na timilifu, yenye utakatifu kinyume cha dhambi na uovu.’ Katika hali hii, ishara za upendo wa Mungu zilikuwa ni wale watu ambao Ashuru waliwakata viungo kama mateka wa ufalme wa kaskazini wa Israeli.

Kama watu wa Mungu katika ufalme wa kusini wa Yuda, tunaweza kuwa na faraja katika kweli kwamba Mungu wetu, ambaye ni asili kamili ya upendo mtimilifu, kwa hakika, ‘atavuka’ na

kudhihirisha hasira yake kwa niaba ya watu wake waliogandamizwa. Yeye atawaangamiza kabisa waovu kupitia dhihirisho kamili la Utakatifu na haki Yake.

SURA YA NANE

Unabii Wa Habakuki

Wale wanaomfahamu nabii huyu mdogo Habakuki, humfikiria kama nabii ambaye hakuwa na majibu, ila tu maswali mengi, mengi sana. Ilionekana kana kwamba alikuwa na akili iliyokuwa imejikunja kama ishara ya swali (?) Katika sura tatu fupi za unabii wake, anamlilia Mungu tena na tena kwa maswali kama 'kwa nini.' Kwa sababu hii, watu wengi wamempa jina 'Nabii Asiyeamini.'

Huyu ni mtu asiyeamini kwamba hatufahamu kumhusu Mungu na maswali ambayo wana filosofia na wasomi wakuu wa thiolojia wamekuwa wakiuliza kwa maelfu ya miaka. Mtu asiyeamini anaelezwa kama anayesema, *'Mimi sijui; wewe hujui, na hakuna ye yote anayejua. Bali ni busara kulifikiria!'* Swali langu kwa asiyeamini wakati wote limekuwa, *'ikiwa ni vigumu kujua, je! Wewe unawezaje kujua kwamba hauwezi kujua?'*

Kwa maoni yangu kuhusu manabii, nilieleza kwamba Mungu aliwaita kutoka kila mahali na tabaka mbali mbali za maisha. Sisi hujifunza kutoka vitabu vya historia vya Agano la Kale kwamba Daudi aliwachagua makuhani elfu nne kwa ajii ya kuimba peke yake, kwa kutumia vyombo ambavyo yeye mwenyewe aliunda kwa ajili hiyo **(1 Mambo ya Nyakati 23:5)**. Walawi hawa wahudumu na waimbaji waliandika Zaburi nyingi sana. Habakuki alikuwa mmoja wa waimbaji hao Walawi. Yeye alikuwa kiongozi wa ibada na nyimbo.

Mnara Wa Habakuki

'Wahubiri huwa wanajibu maswali ambayo hakuna anayeuliza, na kuwakuna ambapo hapawashi.' Wakati mwingi wahubiri ni lazima wakiri hatia kwa shtaka hilo kwa kuwa kuna ushahidi wa kutosha kuwahukumu. Hii haikuwa hali ya Habakuki.

Habakuki alikuwa Yeremia wa siku zile. Alikuwa ameshuhudia kuteswa kwa yule nabii mkuu. Naamini kwamba Habakuki aliamini kwamba, ikiwa watu wa Yuda wangemtendea nabii mkuu kama Yeremia jinsi walivyofanya, basi wangemtendeaje mkuu wa nyimbo ambaye alikiri kwamba alikuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu kwa ajili yao?

Nina ushawishi kwamba Habakuki alibuni aina ya mfumo wa uandishi mwafaka hili kutangaza unabii wake ambao ungemwenzesha kuwa na wasikizaji, na kuwatayarisha watu wa Yuda kulipokea Neno la Mungu alilowapa. Pia nashawishiwa kwamba wakati Habakuki aliuliza maswali haya, alikuwa akiuliza maswali ambayo watu wa Yuda walikuwa wakimwuliza Mungu, na kujiuliza miongoni mwao kila siku.

Watu wa Yuda katika mji wa Yerusalemu walikuwa wakitarajia majeshi ya Babeli wakati wo wote. Vinara vyao vilikuwa na walinzi huku kila mtu akichunga na kusikiza kwa ishara na sauti za Wababeli walioohofiwa sana. Habakuki alitangaza kwamba atajenga 'mnara wa ulinzi' wa kiroho. Yeye angepanda mwenyewe kwenye mnara wa ulinzi, na kumwuliza Mungu maswali (kwa hakika yaliyokuwa ya watu wale) yote. Kisha, angekaa na kulinda, kusikiza na kumngojea Mungu kujibu maswali yake (na yao).

Naamini kwamba watu walimhimiza Habakuki kupanda kwenye 'mnara wa ulinzi' na kumwuliza mswali ambayo yalikuwa mazito mioyoni mwao. Wakati Habakuki alipokuwa kwenye mnara wake wa ulinzi, alimwuliza Mungu sababu ya kutumia mataifa ya waovu - Babeli - hili kuwaangamiza watu waliochaguliwa Wake. Aliuliza: *'Ee Bwana, Mungu wangu, mtakatifu wangu, wewe si wa milele? Hatutakufa. Ee Bwana, umemwandikia hukumu, nawe, Ee Jabali, umemweka imara ili aadhibishwe. Wewe uliye na macho safi hata usiweze kuangalia uovu, wewe usiyeweza kutazama ukaidi, mbona unawaangalia watendao kwa hila; na kunyamaza kimya, hapo mtu mwovu ammezapo mtu aliye mwenye haki kuliko yeye?* **(1:12,13)**.'

Habakuki (pamoja na watu wa Yuda), walikuwa wakifahamu kweli kwamba Mungu alikuwa akiwatumia Wababeli hili kuwaadhibu watu wa Yuda kwa ajili ya dhambi yao, hata hivyo, ilikuwa vigumu kwake (kwao) kuelewa sababu ya Mungu kulitumia taifa la watu waovu hili kuwarudi watu wake. Kwa hakika, yeye (wao) alidhania kwamba, uovu wa Wababeli ulizidi wa watu wa Yuda. Ni kwa sababu gani Mungu alitumia taifa la watu waovu kuwaadhibu watu wake?

Haya ndio yaliokuwa maswali na mazingira ambayo Habakuki alikuwa akiuliza ambayo hayakuwa kwa moyo wake binafsi tu, bali katika mioyo ya wote waliokuwa chini ya hukumu ya watu wa Yuda ukingoni mwa uvamizi kutoka Babeli. Alikuwa akichunguza, kusikiza pamoja na kungojea majibu kutoka kwa Mungu kuhusu maswali yake (yao). Alitangaza: *'Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwangu* **(2:1).'**

Ujumbe Wa Habakuki

Hebu fikiria furaha watu waliokuwa nayo wakati Habakuki alipotangaza kwamba alisikia kutoka kwa Mungu akiwa kwenye mnara wa ulinzi! Je! huu si ni mfumo wa uandishi maalumu ambao nabii huyu alichagua kwa ujumbe huu uliokuwa ukitarajiwa. Habakuki alihubiri kwamba Mungu alikuwa amejibu maswali yake (yao). Ingawa Alikuwa akitumia mataifa maovu kuwaadhibu watenda maovu wa Yuda, Mungu alimjibu Habakuki kwamba Wababeli hawangefanyika kuwa taifa kuu ulimwenguni kwa muda mrefu. Jinsi tumejifunza, milki ya Babeli ilidumu kwa muda wa miaka sabini.

Kwenye mnara wa ulinzi, Mungu alimwambia Habakuki kwamba Babeli walikuwa na mbegu za kuangamia mioyoni mwao. Yeye anaandika kwamba Mungu alimwambia Wababeli walikuwa na mioyo iliyokuwa kombo. Hivyo basi, Mungu alimwambia Habakuki kile Yesu alichofundisha wakati aliposema, *'Maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga* **(Mathayo 26:52).**' Wao wangeangamizwa na ukatili na uovu wao: *'Tazama, roho yake hujivuna,*

haina unyofu ndani yake; lakini nwenye haki ataishi kwa imani yake. Naam, pamoja na hayo, divai ni mchumi mdanganyifu, mtu wa kiburi asiyekaa nyumbani mwake, huongeza tamaa yake kama kuzimu, naye huwa kama mauti, hawezi kushibishwa; bali hujikusanyia mataifa yote; hujiwekea kabila zote chungu chungu **(2:4-5)**.'

Hakika Babeli walikuwa ndio wenye 'kujivuna' ambao Mungu alikuwa imetaja hapa, ambao mioyo yao ulikuwa kombo, au isio sawa ndani. Ni wenye haki tu, au walio na mioyo iliyonyooka - wanaomjua Mungu na kuishi kwa imani katika ahadi zake - wawezao kuishi hivyo **(4).**

'Wenye haki wataishi kwa imani.' Maneno haya yana tafsri moja ilhali matumizi ni mengi. Kwa sababu ya majibu yatokanao na maswali ya Habakuki, Mungu alikuwa akiwaahidi na kuwapa tumaini ya hapo baadaye watu wa Yuda. Ikiwa walikuwa na imani kuwaamini manabii, kama vile Isaya hasa Yeremia, basi wangeishi kama jamii na kurejeshwa katika nchi yao. Hii ilikuwa tumaini ambayo ilimaanisha kwamba taifa la watu waovu halingepata ushindi wa mwisho. Lakini wenye haki wangeishi ikiwa walikuwa na imani dhidi ya ahadi za Mungu ambazo walisikia kupitia manabii waaminifu.

Matumizi yake yanapatikana katika Agano Jipya pale msitari huu wa Habakuki ulikaririwa mara tatu. Mageuzi ya Waprotestante yalianza wakati kasisi wa Kikatoliki kwa jina *Martin Luthe*r alipopata Maandiko haya katika sura ya kwanza ya waraka wa Paulo kwa Warumi, wakati alipokuwa katika maombi yake ya asubuhi **(Warumi 1:17).** Elimu ya thiolojia ya mageuzi ya Kiprotestante yalinakiliwa katika maelezo ya Luther katika nyaraka za Paulo kwa Warumi na Wagalatia, pale ambapo msitari huu unapatikana **(Wagalatia 3:11).** Mahali pa tatu ambapo msitari huu umenakiliwa katika Agano Jipya ni pale tunapoelezwa utangulizi na kumalizia kwa sura kuu ya imani katika Biblia **(Waebrania 10:38)**.

Wimbo Wa Habakuki

Hatuna habari zo zote kuhusu yaliyomkumba shujaa huyu kiongozi wa uimbaji na nabii. Wakati miji kama Yerusalemu ilipoanguka, wakaazi wake waliuawa na walionusurika kuchukuliwa watumwa hadi uhamishoni. Ingawa Habakuki alifahamu kuwa uvamizi na utekaji kutoka Babeli haukuwa mbali, na ungedumu kwa muda wa miaka sabini, alimalizia ujumbe wake kwa wimbo wa sifa. Hakuwa na njia ye yote kufahamu mambo yajayo katika maisha yake, lakini alifahamu kwamba mambo yajayo katika taifa lile yalikuwa yenye matumaini. Yuda ingerejezwa baada ya miaka sabini, Babeli ingeanguka, na Yuda ingeendelea kuwa watu wateule wa Mungu.

Habakuki alianza unabii wake kwa kile kilichoonekana kama kusononeka kwa kukata tamaa na shaka, lakini alimalizia unabii huo kwa wimbo wa sifa, ibada na ulio thabiti. Kwa njia ambayo alimalizia unabii wake, alionyesha watu wa Mungu katika vizazi vyote na kila mila na desturi jinsi ya kusononeka na kukata tamaa kwa kuwa ni wimbo wa sifa.

Wimbo na mfano wa Habakuki wakati anapoandika wimbo huu, unataja kinyume cha mwaminifu ambaye anamtumia Mungu tu. Mwaminifu mwenye kumtumia Mungu ni kama mtu anayetumia vitu kama kwa mfano umeme, maji, au usafiri wa magari ya abiria. Wimbo wa kumalizia wa Habakuki unamweleza mtu wa imani ambaye anamfahamu Mungu, kwamba Hawezi kutupilia mpango Wake wa kumkaribisha Masihi kupitia watu Wake. Ikiwa maneno ya Mungu yalikuwa kweli, jinsi Habakuki alivyoamini, basi watu Wake kwa hakika hawangesahaulika kamwe. Wao wangekwenda uhamishoni, na pia wangeadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao, lakini hawangeangamizwa kabisa ikiwa unabii wa Masihi ungetimika.

Jinsi Mungu alitoa ufunuo wa ajabu kwa Ayubu wakati wa dhiki kuu, na kwa Yeremia wakati alipokuwa anayatunga Maombolezo, Mungu pia alimpa Habakuki wimbo huu mkuu wakati wa giza kuu katika maisha yake. Hapa kuna wimbo huo kwa ufupi.

'Ee Bwana, nimesikia habari zako, nami naogopa;
Ee Bwana, fufua kazi yako katikati ya miaka;
Katikati ya miaka tangaza habari yake;
Katika ghadhabu kumbuka rehema.

Maana mtini hautachanua maua,
Wala mizabibu hamtakuwa na matunda;
Taabu ya mizeituni itakuwa bure,
Na mashamba hayatatoa chakula;
Zizini hamtakuwa na kundi,
Wala vibandani hamtakuwa na kundi la ng'ombe;
Walakini nitamfurahia Bwana.
Nitamshangilia Mungu wa wokovu wangu.
Yehova, aliye Bwana, ni nguvu zangu,
Yeye huifanya miguu yangu kuwa kama ya kulungu,
Naye ataniendesha katika mahali pangu palipoinuka
(Habakuki 3:2; 17-19).'

(Mwongozo kwa kiongozi wa nyimbo: Wakati wa kuimba aya hizi, waimbaji wanahitaji kuwa na vyombo vya kamba vya uimbaji).

Matumizi Ya Kibinafsi

Ingawa wachache wetu hukumbana na pingamizi kama zile zilimkumba Habakuki, wakati tupokuwa na shida zinazotuvuruga, huwa na uwezo wa kuelekeza nguvu zetu za kimwili, hisia, na kiroho katika shida yetu, au kujenga mnara wa ulinzi wa kiroho na tunaweza kuchungulia hadi tumwone Mungu jinsi anavyotenda kazi katika maisha yetu. Tunaweza kusikiza hadi tutakaposikia kutoka kwa Mungu jinsi anavyotenda kazi maishani mwetu. Tena, kama Habakuki, tunaweza kumwabudu Mungu ambaye anatenda kazi maishani mwetu.

Je! Wewe umewahi kujenga mnara wa ulinzi wa kiroho - mahali ambapo unamchungulia na kutazama, kungojea hadi utakaposikia kutoka kwa Mungu? Kitabu cha Habakuki kinatufundisha kwamba tunahitajika kujenga mnara wa ulinzi na kumwendea Mungu kwa maswali yetu. Yeye atatujibu kwa wakati wetu wa kimya tunapomtazamia, kumsikiliza na kumngojea. Mchungaji moja alisema hivi: 'Nimeambiwa kwamba Mungu hazungumzi na watu wake siku hizi jinsi ilivyokuwa na Habakuki. Ingekuwa sawa kusema kwamba watu wa Mungu hawamsikilizi jinsi ilivyokuwa siku za mtu huyu mwenye karama na mwimbaji mashuhuri.

SURA YA TISA

Unabii Wa Sefania

Kama nabii Yoeli, Sefania alikuwa nabii wa Siku ya Bwana. Ingawa alitilia mkazo siku ya Bwana kwa wakati uliopita, wa sasa, na ujao, Sefania alitilia mkazo unabii wake kwa siku ya mwisho ya Bwana ambayo itakuwa mojawapo ya mambo ya mwisho ambayo Yesu, manabii na mitume walitufahamisha.

Yaliyomo Katika Siku Ya Bwana (Sura 1)

Wakati Sefania alipohubiri kuhusu siku ya Bwana, alieleza kuhusu matukio ya uharibifu mkuu yatakayokumba ulimwengu kila mahali pa uumbaji. Kupitia Sefania, Mungu alitangaza, *'Nitavikomesha kabisa vitu vyote, visionekane juu ya uso wa nchi, asema Bwana. Nitamkomesha mwanadamu na mnyama; nitakomesha ndege wa angani, na samaki wa baharini, na hayo makwazo pamoja na wabaya; nami nitamkatilia mbali mwanadamu, asionekane juu ya uso wa nchi asema Bwana* **(1:2-3).'**

Kulingana na Sefania, Siku ya Bwana itakuwa ya mwisho na yenye mabadiliko makubwa katika maumbile. Hii haitahusu tu wana wa Yuda na watekaji nyara wao wa Babeli; bali pia itahusisha wanadamu wote, wanyama pamoja na ndege na samaki wa baharini.

Sawa na manabii wengine, Sefania alichanganya unabii wake wa Siku ya mwisho ya Bwana na unabii kuhusu uvamizi kutoka Babeli wakati alipozungumza haya maneno ya Mungu katika misitari ifuatao: *'Nami nitaunyosha mkono wangu juu ya Yuda, na juu ya watu wakaao Yerusalemu; nami nitayakatilia mbali mabaki ya Baali, yasionekane mahali hapa, na hilo jina la Wakemari pamoja na makuhani. . . Na itakuwa, katika siku ile ya dhabihu ya Bwana, nitawaadhibu wakuu na wana wa mfalme, na watu wote waliovaaa mavazi ya kigeni. Na katika siku ile nitawaadhibu hao wote warukao juu ya kizingiti, waijazao nyumba ya Bwana wao wa udhalimu na udanganyifu* ***(1:4; 8-9).'***

Sefania alijiunga na nabii Mika kutilia mkazo lawama na hukumu juu ya viongozi wa kiroho na kisiasa wa Yuda kwa uasi wao kiroho na ufisadi wa tabia za watu. Na kama matokeo ya dhambi za viongozi hao, Mungu alikuwa akileta hukumu juu ya jamii yote, kulingana na manabii wadogo. Hukumu hii ya Mungu kutoka kwa viongozi hadi kwa watu wa kawaida inaonyesha jinsi Mungu anatilia mkazo juu ya wajibu wa viongozi mbele Zake kwa ajili ya wema wa watu walio chini yao.

Asili Ya Siku Ya Bwana (Sura ya 2)

Ingawa Sefania alitangaza hukumu ya Mungu kwa Yuda kwa sababu ya dhambi zake, pia alitabiri kuhusu Siku ya Bwana itakayowajia mataifa yote, hasa yale ambayo yaliwatesa wana wa Yuda: *'Na katika Siku Kuu Ile na ya Mwisho, watu wote wa ulimwenguni watawajibika kwa matendo yao humu duniani, naye Mungu ndiye atakayekuwa mwamuzi wa mwisho. Sefania alitangaza kwamba wale tu wamwabuduo Mungu mmoja aliye wa kweli katika maisha yao ndio watakaoepuka ghadhabu Yake siku ile ya mwisho.'*

Katika hali ya kweli, Sefania aliyashauri mataifa kutubu: *'Jikusanyeni, naam, jikusanyeni, Ee taifa lisilo na haya; kabla haijazaa hiyo amri, kabla haijapita siku ile kama makapi, kabla haijawajilia hasira kali ya Bwana, kabla haijawajilia siku ya hasira ya Bwana. Mtafuteni Bwana, enyi nyote mlio*

wanyenyekevu wa dunia, ninyi mliozitenda hukumu zake; itafuteni haki, utafuteni unyenyekevu; huenda mtafichwa katika siku ya hasira ya Bwana **(2:1-3).**'

Ingawa yale mataifa ya wasiomcha Mungu yalitumiwa hili kuwarudi Yuda, wao hawakuwa wana wa Mungu Aliye wa kweli ambaye yu hai. Sefania aliwaita kwa toba hili kuwaokoa kutokana na moto ambao Mungu atauleta Siku ya Mwisho ya Bwana.

Jambo kuu katika Siku ya Bwana itakuwa ni dhambi na uovu wa mataifa. Katika maelezo yake kati ya watu wa Yuda na wa mataifa yasiyomcha Mungu, Sefania aliorodhesha dhambi na fanaka, kama kutojali, kutotii, kuasi na kutomcha Mungu. Dhambi hizi za watu wa Mungu na wa mataifa yasiomcha Mungu zitazua ghadhabu Yake na kuwa chanzo kikuu cha Siku Kuu ya Bwana, kulingana na Sefania.

Sefania pia anatabiri kwamba hukumu ya Mungu itayaangukia mataifa yote yaliyomo kando mwa ukingoni mwa bahari, na kwamba, *' hiyo nchi ya pwani itakuwa nchi ya watu wa nyumba ya Yuda waliosalia; watalisha makundi yao huko . . . kwa maana Bwana, Mungu wao, atawajilia na kuwarudisha wafungwa wao* **(7).'** Pia, alihubiri kinyume cha Moabu na Amoni, pamoja na Wakushi na Ashuru, atatenda haya yote hili kuonyesha kwamba watu wasiomcha Mungu hawataiepuka hukumu ya Bwana.

Kiumbe Kipya Katika Siku Ya Bwana (Sura ya 3)

Ingawa Sefania alikemea Yuda kwa ajili ya viongozi wafisadi na kuwa pingamizi kinyume na Mungu **(3:1-4)**, na kutangaza kwamba uvamizi kutoka Babeli ni matokeo ya matendo yake, pia alizungumzia kuhusu tumaini ambalo Yuda ingechukua hadi Siku ya mwisho ya Bwana. Katika siku ile, mataifa yote duniani yatamkiri Bwana kama Mungu **(8-11),** nao waliosalia kutoka Israeli watapatikana wale walio waaminifu: *'Mabaki ya Israeli hawatatenda uovu, wala kusema uongo; wala ulimi wa hadaa hautaonekana kinywani mwao; kwa maana watakula na kulala, wala hapana mtu atakayewaogofya* **(13).'**

Licha ya kushindwa kwa watu wa Yuda kubaki wakiwa waaminifu kwa Mungu, Sefania alitabiri kwamba Mungu atawahifadhi, na kuwaita kutoka utumwani hadi Siku za mwisho, waliosalia waaminifu, watabaki hata milele Kwake, viumbe vipya. Tunauona unabii ukitimizwa kwa sehemu moja katika vitabu vya historia vya Ezra na Nehemia, na katika manabii watatu wa mwisho ambao tutawakachambua katika masomo yetu. Hawa ni manabii wa baada ya uhamisho na uvamizi wa Babeli waliowahudumia mabaki ya wale waliokuwa uhamishoni huko Babeli.

Kwa kuwa unabii wa Sefania unatilia mkazo Siku ya mwisho ya Bwana, wengi wanaamini kwamba unabii wake kuhusu mabaki ambao watakuwa wanyenyekevu, wapole, na wenye haki, umetimika katika Kanisa la Yesu aliyefufuka ambaye anayeishi. Mitume wote walikuwa Wayahudi, naye Paulo anaandika kwamba watu wote wa mataifa ambao wamezaliwa kwa mara ya pili ni wana wa Ibrahimu (**Wagalatia 3:7).** Paulo anafanyika kuwa nabii wakati anapotabiri kwamba Mungu atarudisha taifa la Kiyahudi kwake mwenyewe na *'Israeli yote itaokolewa* **(Warumi 9-11)**.'

SURA YA KUMI

Unabii Wa Hagai

Manabii wale wote ambao umesoma waliishi na kuhubiri kabla, au wakati wa utumwa huko Babeli. Manabii Hagai, Zekaria, na Malaki wanaitwa ‘manabii wa baada ya utumwa’ kwa kuwa walihubiria Wayahudi wale waliorudi kutoka Babeli. Vitabu kumi na viwili vya historia katika Agano la Kale vinatupatia utangulizi na hali iliyokuwepo wakati manabii hawa waandishi walipoishi na kuhubiri. Ili kufahamu vyema hali ya kihistoria ya manabii hawa watatu wa mwisho, itakuwa bora ikiwa unaweza kusoma kitabu cha Ezra, au kile kilicho na maelezo juu ya vitabu vya historia **(kitabu cha 3 na 4),** ambacho kitakukumbusha ulichojifunza kuhusu kurudi kwa hatua tatu tofauti kutoka uhamishoni Babeli.

Hagai na Zakaria waliwahubiria wale waliokuwa katika kundi la kwanza kurudi kutoka Babeli. Kundi la kwanza lilitokea punde tu baada ya kuanguka kwa ufalme wa Babeli mikononi mwa Wamedi na Uajemi. Kundi hili la kwanza lilikuwa na mwongozo mwafaka wa kazi. Mwongozo wa maono ya kundi ili ulikuwa ni kulijenga upya Hekalu la Sulemani. Lengo kuu la mwongozo huo litakuwa ndio moyo na roho ya jumbe za manabii Hagai na Zekaria.

Katika utimizaji wa unabii wa kimuijiza wa Isaya, Koreshi Mkuu, mfalme wa milki ya Uajemi, ilitoa amri ya kifalme akiwapa ruhusa watumwa pamoja na vyombo ili kulijenga Hekalu. Ingawa kurudi huko kulijenga Hekalu kulikuwa mwuijiza mkuu, hakukuwa na ukuu au utukufu wo wote.

Takribani wakimbizi hamsini elfu wadhaifu ndio waliorudi kulijenga Hekalu. Inawezekana kwamba wao walionekana kama wakimbizi tunaosikia na kuwaona siku hizi.

Wakati mmoja, walikuwa ni jeshi la watu laki sita (600,000) ambao waliohofiwa sana na maadui zao kama wale waliokuwa wakiishi kwenye miji iliozungukwa na kuta kubwa huko Kanaani **(Yoshua 2:9-14).** Na sasa wao hawana jeshi wala taifa. Zaidi ya hayo, walishtuka na kukata tamaa walipogundua kwamba nchi yao ilikuwa imenyakuliwa na watu wa mataifa ambao hawakuwatakia mema. Yamkini sasa mtazamo wetu wa kihistoria ni bora katika kuelewa changa moto zilizowapata manabii hawa Hagai na Zekaria.

Ujumbe Wa Hagai

Watu ambao wakimbizi hawa waliwapata wakiishi huko Yerusalemu na Yuda ni wale waliokuwa wametekwa na ufalme wa Babeli na kuhamishwa kutoka nchi zao hadi nchi ya Yuda. Wao waliupinga ujenzi wa Hekali sana. Huku wakishawishika kwamba nguvu zile zilizowafanya Wayahudi kuwa taifa kubwa ziko katika Hekalu lile, waliwadhulumu na kuwatesa watu wa Yuda wakati ujenzi ulipoanza. Watu wa Yuda walitishwa sana na upinzani huo wenye chuki hivi kwamba kwa muda wa miaka kumi na tano, wao waliacha ujenzi wa Hekalu lile! Baada ya kufedheheshwa kabisa kutokana na lengo kuu lao, walijitosa katika ujenzi wa nyumba zao. Hapa ndipo anapoingia nabii Hagai!

Unaweza kukumbuka kwamba wajibu wa nabii ulikuwa ni kuipaza sauti kinyume cha kizuizi cha kazi ya Mungu hadi kitakapoondolewa na kazi ya Mungu itimizwe tena. Kazi ya Mungu wakati wa Hagai ilikuwa kujenga Hekalu. Kupotoshwa kwa mwelekeo na nia ya watu wa

Yuda ilikuwa ndio shida-pingamizi iliyokwaza kazi ya Mungu. Hagai alifanya mahubiri manne makuu ambayo yalizungumzia kuhusu Hekalu lile.

Ujumbe Wa Kwanza Wa Hagai: 'Tilia Mkazo Kipao Mbele Chako! (Sura Ya 1).'

Nusu ya kitabu hiki cha Hagai kinanakili, tena kueleza matokeo ya ujumbe wa kwanza wa Hagai. Katika ujumbe huu, Hagai aliwapa watu wa Yuda changa Moto: *'Zitafakarini njia zenu!'* Ujumbe wa Biblia yote unaweza kufupishwa kwa maneno haya mawili: *'Mungu Kwanza!'* Changa moto ya Hagai kwa wakimbizi hawa ilikuwa *'tafakarini wakati wenu na wa Mungu. Mnao wakati kwa ajili ya nyumba zenu, lakini hamna wakati kwa ajili ya nyumba ya Mungu.'*

Akizungumza kwa niaba ya Mungu, Hagai baadaye alihubiri hivi: *'Zitafakarini njia zangu! Mlitazamia vingi, kumbe vilitokea vichache, tena mlipovileta nyumbani nikavipeperusha. Ni kwa sababu gani? Asema Bwana wa majeshi. Ni kwa sababu ya nyumba yangu inayokaa hali ya kuharibika, wakati ambapo ninyi mnakimbilia kila mtu nyumbani kwake* **(1:9)**.' Tafsiri nyingine inasema kwamba walikuwa wakiweka fedha zao katika mifuko iliyotoboka-toboka. Wakati nabii alipowapa changa moto ili waitafakari njia Yake, Neno kutoka kwa Mungu ni kuwa Yeye ndiye aliyekuwa akitoboa mashimo kwenye mifuko yao.

Hagai anawapa wakimbizi hawa changa moto kwamba watafakari yale wanayotenda, na yale Mungu anatenda. Na kama matokeo ya ukuu wao uliopotoka, Mungu aliwaletea baa la ukavu katika kila kazi yao na kwa watu wa Yuda **(10,10).** Hakuwapa mvua ila ukavu na njaa. Kazi yao ngumu haikuwa na mazao; jambo ambalo ni matokeo ya kukataa kumfanya Mungu kuwa wa kwanza.

Ni lazima kwamba Hagai alikuwa mhubiri mwenye ushawishi mkuu kwa kuwa watu hawa walisisimka kwa utiifu. Walidhamini malengo yao na kurejea kazini katika Hekalu. Ujumbe wa kwanza wa Hagai kwa kweli ulikuja katika sehemu kadhaa. Sehemu ya pili ilikuwa ni kuhusu kutii kwao. Shina la sehemu ya pili lilikuwa: *'Mimi nipo pamoja nanyi,* asema Bwana! **(13).** Punde tu walipopanga majukumu yao vema, Mungu alikuwa pamoja nao. Mungu aliwabariki pamoja na kazi zao wakati walipomweka kwanza.

Ujumbe Wa Pili Wa Hagai: 'Elekeza Mtazamo Wako (2:1-9)'

Hekalu la kwanza la Sulemani lilijengwa kwa vyombo vye thamani kuu, kama dhahabu, fedha, na lulu. Utukufu wote uliokuwa wa Sulemani pamoja na utajiri wake, ndio uliodhamini vyombo vile vilivyohusika katika ujenzi wa Hekalu la kwanza. Wakati mabaki ya watu wa Yuda walipojenga lile Hekalu la Sulemani, wao walikuwa wakimbizi maskini. Mali na vyombo walivyokuwa navyo kwa ajili ya ujenzi wa Hekalu ni rasilmali kutoka magofu yaliyobakia katika Hekalu la kwanza, au yale yaliyopewa na mfalme wa Uajemi, Koreshi Mkuu.

Wengi miongoni mwa wajenzi wa Hekalu la pili hawakuwa wameliona Hekalu la kwanza, kwa kuwa walizaliwa huko utumwani. Wale waliokuwa wazee miongoni mwao ambao waliliona Hekalu la kwanza hawangefanya cho chote ila tu kuomboleza kuhusu Hekalu ambalo halingefikia ule utukufu wa kwanza **(Ezra 3:12,13).**

Katika ujumbe wa pili wa Hagai, nabii huyo alihusika na kukumbana na huzuni pamoja na kukata tamaa wakimbizi wazee walioshuhudia. Hagai aliwakumbusha kwamba umuhimu wa Hekalu lile ulikuwa wa kiroho wala sio wa kirasilmali au mambo yanayoonekana kwa macho haya. (Hema la Ibada huko nyikani haikuwa ni ya mawe!) Hagai pia aliwakumbusha hawa wakimbizi kwamba Roho wa Mungu alikuwa pamoja nao.

Ujumbe wa pili wa Hagai uliwaeleza haja la watu kuelekeza mtazamo wao. Neno hili 'mtazamo' linamaanisha, 'kutazama kabisa.' Kuna wakati ambao Maandiko yanatuhimiza kuwa na aina ya 'maono ya bomba' ambayo kinyume na vizingiti na vurugu ye yote, mtazamo wako ni sahihi kwa wakati huu, na wakati ujao, kwa kile Mungu anachotaka sisi kutenda kwa ajili Yake. Hili ndilo lililokuwa shina la ujumbe wa pili wa Hagai.

Ujumbe Wa Tatu Wa Hagai: 'Elekeza Kusudi Lako (2:10-19).'

Baada ya Waebrania kuanza kazi yao ya ujenzi wa Hekalu, walitaka kuona kwa mara hiyo baraka juu ya kazi ile ambayo Mungu alikuwa amewaahidi kupitia sehemu ya pili ya ujumbe wa kwanza wa Hagai. Walitenda kazi kwa miezi mingi, wakati wa baridi kuu na wakati wa hari, na hawakuwa wamepokea baraka hiyo waliokuwa wakitarajia.

Hagai aliwapa watu hao waliokuwa wamekata tamaa maswali mawili. Kwa kuwa makuhani walikuwa wamejibu maswali ya watu kuhusu Maandiko, yeye aliyaelekeza maswali hayo kwa makuhani. Kwanza, aliuliza hivi, *'Ikiwa mtu ataibeba nyama iliyo takatifu katika mavazi yake, je! Vitu vile atakavyovigusa vitakuwa ni vitakatifu?* Kwa swali hili, makuhani walijibu hivi, *'La! sivyo.'* Pili, akawauliza hivi, *'Ikiwa mtu ni najisi, je! Vitu vile ambavyo atagusa vitafanyika najisi?'* Na kwa swali hili wale makuhani wakajibu, *'la! sivyo.'*

Kile walichohitaji kufahamu ni kwamba, utakatifu haushirikishi mara moja, kama vile magonjwa yalivyo. Dhambi hushirikishwa hivyo bali huchukua muda kabla ya kufanyika mtakatifu. Ikiwa baraka zingetolewa sababu yetu kuwa watiifu, basi baraka za Mungu pia zingetolewa haraka kwa ajili ya utiifu wetu, na hivyo basi hizo za Mungu zingekuwa ni matokeo ya kazi zetu, wala siyo neema Yake. Kusudi au azimio letu kwa utakatifu linahitajika kuwa sababu ya stahi au unyenyekevu wetu kwa Mungu, wala sio tamaa yetu ya baraka. Katika ujumbe wa tatu, Hagai aliwapa changa moto kuelekeza azimio yao ya kumtumikia Mungu katika ujenzi wa Hekalu.

Ujumbe Wa Nne Wa Hagai: 'Zielekeze Hofu Zako (2:21-23)'

Waliporudi huko Yerusalemu, hawakuwa na uwezo wo wote wakujilinda baada ya miaka sabini ya utumwa kwani walikuwa wangali na hofu ya kuvamiwa na kufanywa watumwa na mataifa mengine tena.

Ujumbe wa Hagai wa nne ulikumbana na hofu zao. Yeye alitabiri mapinduzi ya Mungu kwa mataifa yale waliokuwa wakihofia pamoja na mpango Wake kutetemesha mbingu na dunia.

Katika ujumbe huu wa nne, Hagai alitabiri kwamba Mungu ataitetemesha nchi hadi vitu visivyoweza kutetemeshwa vikae. Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania ananukuu kutoka ujumbe wa pili wa Hagai na kutuambia kwamba tumepokea ufalme ambao hauwezi kutetemeshwa **(Waebrania 12:26-29)**. Hiki ndicho kina kikuu cha ujumbe wa nne wa Hagai.

Matumizi Ya Kibinafsi

Jumuisha mahubiri ya huyu nabii mkuu katika maisha yako siku ya leo. Je! Thamani zako ni zipi? Je! Mungu anaibariki kazi yako? Na Je! Uko vipi katika maisha yako ya kiroho?

Sehemu mbaya katika hukumu ya Mungu juu ya thamani zilizopotoka kwa hawa wakimbizi ilikuwa kwamba Mungu alikuwa amewaletea baa la njaa katika kazi za mikono yao. Je! Umewahi kujihisi kana kwamba unapitia kwenye baa la njaa katika maisha yako? Ikiwa Mungu haibariki kazi ya mikono yako, na ikiwa unajipata katika sehemu zenye ukavu, basi ujumbe wake hagai kwako wa kutekelezwa ndio huu: 'Zitafakari njia zako,' kisha 'uzitafakari njia za Mungu.'

Je! Mtazamo wako ni upi? Je! Una maono mema yaliyo katika bomba? Je! Kila mara unatazama nyuma na kulinganisha kazi ya Mungu iliyopita katika maisha yako na wakati Mungu anataka utilie mkazo kazi ambayo Anaitenda leo na kesho?

Je! Azimio lako ni lipi katika kumtumikia Bwana? Je! Wewe unatafuta baraka za wakati ule ule unapomtumikia Bwana? Je! Wewe unatenda kazi ya Bwana kwa kuwa unatarajia thawabu papo hapo?

Je! Hofu yako ni gani? Hagai anaungana na Petro kukuhakikisha kwamba unaweza kutupilia mbali fedheha zako kwa Yeye kwa kuwa Anakujali **(1 Petro 5:7).** Kwa kuwa umesoma unabii wa Hagai, achilia imani yako izielekeze thamani, mtazamo, kusudi au azimio pamoja na hofu zako.

SURA YA KUMI NA MOJA

Unabii Wa Zekaria

Huku Hagai akihubiri jumbe zake nne zenye uwezo mkuu, yamkini unaweza kumsikia nabii mchanga Zekaria akimwambia hivi, *'Lakini Hagai, wakati wale wasio na ulinzi na wadhaifu hawana na njia ya kujilinda wenyewe; wakati wale wasio na tumaini na wenye kukata tamaa wamefikia mahali wanakata tamaa; wakati watu wasioweza kujisaidia na wale walioshindwa wakiwa na hofu na kutishwa na dhiki; watu hao wanahitaji kusikia zaidi ya maneno kwamba, 'Iweni na nguvu na tendeni kazi! Wakati watu wamekata tamaa kwa kuwa wanapitia vikwanzo fulani au kwenye msiba, yale wawezayo kuona ni hali ile ya pingamizi tu.'*

Manabii waliitwa 'waonaji' kwa kuwa wangeweza 'kuona' Mungu akitenda kazi huko nyuma, mbele, na katika pingamizi fulani. Mwonaji aliyaona yale ambayo wengine hawangeweza kuona kwa kuwa alimwona Mungu. Zekaria ni mfano bora wa 'mwonaji' katika Biblia.

Zekaria aliamini kwamba watu hao wa Yuda waliokuwa wamevunjika moyo walihitaji maono ya Mungu mweza yote, ambaye alikuwa pamoja nao na angeweza kuwapa nguvu pamoja na kupigana kwa niaba yao. Mungu alitumia mahubiri ya Zekaria kuwapa waliokuwa wameshindwa na kuvunjika moyo, pamoja na wakimbizi waliokata tamaa aina ya maono ambayo yalikuwa Yake mwenyewe.

Mfumo Wa Uandishi Wa Zekaria

Kiini cha unabii wa Zekaria ni maono manane ambayo yeye alishiriki na wakimbizi pamoja nasi pia. Anatilia mkazo juu ya shida ambayo ilikuwa ndio kina cha kuvunjika moyo na kukata tamaa kwa manusura hawa Wayahudi kutoka utumwani. Kisha ataivuta pazia ya kufikirika na kushiriki nasi maono ya jinsi Mungu anatenda kazi kinyume cha pingamizi iliyopo. Atatenda hivyo kwa mara nane katika unabii huu wenye nguvu. Huu ndio mfumo wa uandishi wa Kitabu cha Zekaria.

Ujumbe Wa Zekaria

Ujumbe wa Mungu kupitia Zekaria ulikuwa, *'Rudini kwangu mimi . . .Nami nitawarudieni ninyi.'* Jinsi walivyo Wayahudi katika Israeli ya siku ya leo, hawa wakimbizi walikuwa wakishiriki katika kurudi kwenye nchi yao kuliko kutabiriwa na manabii kadhaa. Kupitia mahubiri yake Zekaria, Mungu alikuwa akiwauliza watu hawa kurejea kwao kiroho, wala sio katika mji au Hekalu, bali kwa Mungu mwenyewe. Hali kuwa jambo hili halijatukia kwa Wayahudi wa siku ya leo, Zekaria na manabii wengine pamoja na mtume Paulo, wanatabiri kuhusu kurudi kwao kiroho wakati, *'Israeli yote itakapookolewa* **(Zekaria 8:20-23; Warumi 11:26; Isaya 59:20, 21).'**

Yamkini mara hamsini na tatu Zekaria anatumia msemo, 'Bwana wa majeshi' ambao unamdhihirisha Mungu kama Bwana wa majeshi ya malaika na nyota pamoja na nguvu zote za asili ambazo Yeye hutumia katika kutekeleza makusudio Yake humu duniani. Kuna njia ambayo msemo huu unajumuhisha utabiri wote wa Zekaria kwa kuwa maono yake yote yatatueleza kwamba alimwona Mungu kama 'Bwana wa majeshi' wakati watu wa Mungu walipokuwa wadhaifu katika hali ya ulinzi na kisiasa.

Zekaria alimwona Bwana wa majeshi akitenda kazi kwa njia tatu kwa niaba ya watu Wake. Kwanza, kulikuwepo na Bwana wa majeshi Mwenyewe. Pili, njia iliyo muhimu sana ambayo Mungu atakutana na mahitaji ya watu Wake hili wamjie kupitia kile ambacho Zekaria anataja kama 'tawi.' Isipokuwa sura zile sitini na sita za Isaya, sura hizi kumi na nne za Zekaria zina unabii wa Masihi zaidi ya nabii mwingine. Wakati Masihi alipokuja kutimiza unabii wa Zekaria, Kristo aliwaambia watu Wake wazi kwamba, *'Mimi ndimi njia (kurudi kwake Mungu) . . . na hamna mtu awezaye kumjia Baba isipokuwa kwa njia yangu!* **(Yohana 14:6).'**

Njia ya tatu ambayo Zekaria alihubiri kwamba Mungu atarudi na kuturudisha Kwake ndio ahadi ifahami-kanayo sana ya Kipentekoste: *'Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi* **(4:6).'**

Kwa njia hii, Zekaria alichora picha ya kuvuita ya Utatu wa Mungu. Bwana wa Majeshi ni Mungu Baba; njia ya kumrudia Mungu Baba ni kupitia kwa Tawi, Ambaye ni Mwana. Wakati watu wa Mungu watakaporudi kwa Mungu kwa njia ya Mwanawe, Atawapa uwezo wa Kipentekoste kutoka kwa Roho Mtakatifu.

Maono Nane Ya Zekaria

Neno 'Ufunuo' maanake ni, 'kuvuta nyuma pazia na kudhihirisha kile ambacho hakingejulikana kwa njia nyingine.' Zekaria anavuta nyuma pazia ile mara nane na kuwaonyesha watu wa Mungu kile ambacho Mungu alikuwa akitenda hapo kwa njia ambayo mambo

yalivyoonekana kuwa. Mungu alimpa Zekaria maono haya hili kuwatia nguvu watu Wake waliokuwa wadhaifu, na kuwapa tumaini waliokuwa wamekata tamaa.

Maono Ya Kwanza: 'Maono Ya Mahali Penye Uvuli (1:7-17)'

Kulingana na wasomi wengi wa Biblia, mtu aliyekuwa akisimama katikati ya miti kwenye bonde ndogo anawakilisha ushuhuda mgumu katika mabadiliko yaliokuwa sehemu ya wale wakimbizi. Wakati huu wa mabadiliko kati ya kurejeshwa kwao kwa njia ya miujiza kutoka utumwani huko Babeli, na changa moto ya kubadilisha magofu ya uharibifu kuwa Hekalu; ulikuwa wakati wenye kushusha moyo sana kwa wale watu. Kwa maelezo mengine, walijipata chini kwenye bonde. Shida-pingamizi iliyoonekana 'kabla ya ile pazia' ilikuwa ya kuvunja moyo kwani ilikuwa kweli kwamba wao walikuwa si taifa, bali watu wasio na utaratibu wenye kuhurumiwa, yaani kundi la wakimbizi. Walikuwa katika yakati mbovu, za kuogofya za ushuhuda wa mabadiliko ambao sote hupitia.

Wakati Zekaria alipoivuta ile pazia, aliona kile alichotaja kama 'mtazamaji', ambaye alikuwa Bwana wa Majeshi. Mungu alifahamu na alikuwa akitazama yale mabadiliko ya watu Wake. Hata hivyo, Mungu alikuwa kwa njia ya miujiza, ndiye ameumaliza utumwa wa watu Wake. Kwa wakati wake na kulingana na njia yake, Mungu atatimiza mpangilio Wake kwa kurejeshwa kwao kwa ukamilifu katika nchi yao roho zao Kwake.

Mungu atakapokufanya kitu kipya katika maisha yetu, wakati atakapotuita mahali papya, wengi wetu na wakati mwingi, huweka vikwazo vitatu. Kwa kuwa misingi yetu mikuu ni kuwa sisi tu viumbe vitafutao usalama, hatupendi kuacha viota vyetu vilivyo na usalama ambavyo tunaishi na kuhudumu wakati huu. Hivyo, ni lazima Atuondoe mahali pa kale kabla hajatuongoza mahali papya. Hii ndio sababu wakati wote mwito wa Mungu huwa na maeneo mawili - mvuto kutoka mbele na msukumo kutoka nyuma. Kwa maelezo mengine, Mungu ni lazima atulipue kutoka huko tulimo ili aweze kutuongoza katika upya. Je! Unaweza kufikiria nyakati ambazo Yeye alitenda muijiza huo kwako? Naitaja miujiza hiyo kama 'tendo la Mungu.'

Wakati sisi tupo katikati ya yale ya kale na mapya, Mungu wetu ni lazima atuendeleze hili aweze kutuvukisha vyema katika mabadiliko yetu. Ni lazima atufanye kuwa sawa hili aweze kutuweka mahali papya na katika jambo jipya ambalo Yeye anataka kulifanya katika maisha na huduma zetu. Wakati wana wa Israeli walipokuwa kule Misri na Mungu akataka wao kwenda katika Nchi ya Ahadi, Aliueleza muijiza huo kwa njia hii: *'Akatutoa huko ili kututia huku, apate kutupa sisi nchi aliyowaapia baba zetu* **(Kumbukumbu la Torati 6:23).'**

Maono Ya Pili: Pembe Nne (1:18-21)

Katika Biblia, pembe ni ishara ya Uwezo. Shida-kikwazo kilichokuwepo mbele ya pazia ambayo ilikuwa ikilisha hofu zao ilikuwa nguvu za kutisha kutoka mataifa ya ulimwengu ambao yaliwateka na kuwahamisha hadi nchi ya utumwa wakati walipokuwa taifa lenye uwezo. Mataifa yenye nguvu yangali yanawavamia na kuwachukua mateka hadi utumwani.

Wakati Zekaria aliondoa pazia, kile alichoona nyuma yake na kuwaonyesha wakimbizi hao kiliwapa ujasiri na tumaini. Nyuma ya pazia lile, Zekaria alidhihirisha mataifa makuu ya ulimwengu ambayo Bwana wa Majeshi alikuwa atumie kuangamiza zile 'pembe' au mataifa makuu yaliowatisha ambayo alidhania kwamba yangewavamia na kuwateka.

Maono Ya Tatu: Mji Wa Yerusalemu (2:1-2, 10-13)

Shida iliyoonekana mbele ya pazia ilikuwa kile kifusi cha mabaki ya kile kilichokuwa hapo awali mji wa kuvutia wa Yerusalemu. Wakati Zekaria alipoifungua ile pazia, kile alichoona nyuma yake na kudhihirisha watu kilikuwa ni mji wa Yerusalemu wenye kuvutia uliojengwa upya. Ufunuo huu ulidhihirisha kwao kwamba kile ambacho kwa sasa kilikuwa kifusi kingefanyika kuwa mji mkuu ambao haungeweza kulinganishwa, wenye ulinzi bora kutoka kwa Bwana wa Majeshi na Yerusalemu haikuhitaji kuta zo zote.

Yerusalemu na Hekalu zilirejeshwa na kuwa mji na Hekalu ambalo lilitembelewa sana na Yesu. Miaka arobaini baada ya Yesu, Warumi waliharibu kabisa mji huo pamoja kubomoa kabisa kuta zake na kuwa jinsi ulivyo hata siku ya leo. Sherehe iliyofuatia dhabihu za wanyama ilitupiliwa mbali wakati Warumi walipoharibu mji wa Yerusalemu mnamo mwaka wa 70 baada ya kuzaliwa kwake Yesu Kristo. Ingawa sehemu moja ya unabii huu wa Zekaria ilitimizwa wakati Yerusalemu iliporejeshwa na ujenzi ukaanza kabla ya Kristo, kwa mara nyingine baada ya uharibifu huo wake kutoka kwa Warumi, kutimika kikamilifu kwa unabii huo kutatokea katika Yerusalemu Mpya ambayo inaelezwa kiunabii na Mtume Yohana **(Ufunuo 21:2).**

Maono Ya Nne: Mshtaki Wa Ndugu (3:1-2; 8-10)

Shida ambayo Zekaria aliagazia kabla ya pazia iliyowashusha moyo wakimbizi ilikuwa ni maono ya Yoshua, kuhani wao mkuu ambaye alikuwa amevalia mavazi machafu. Katika maono haya, Shetani alikuwa akimshtaki Yoshua. Mawaa mabaya kutokana na ile dhambi ya kuabudu sanamu ambayo ilikuwa tayari imeondolewa na kusamehewa kupitia ushuhuda wa uhamisho, yamkini ndio sababu kuu iliotiwa mkazo katika mashtaka ya yule muovu.

Mshtaki Shetani hutumia matokeo au mawaa ya dhambi ambazo zimesamehewa hili kuwashtaki ndugu usiku na mchana. Tunaambiwa katika kitabu cha Ufunuo kwamba wakati kazi ya huyu muovu itakapotamatishwa, hapo ndipo wokovu, uwezo na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo yatakuja **(Ufunuo 12:10).**

Wakati Zekaria anafungua ile pazia, anaona na kudhihirisha kwa watu, Ufunuo wa Utatu Mtakatifu - Bwana wa Majeshi, na dhihirisho la upendo na uwezo wa Mungu unaowajia kupitia Masihi ambaye anamtaja kama 'wakili.' Pia anamwona Roho Mtakatifu, na miujiza ya hapo baadaye ambayo itakuwa sehemu ya mjio wa pili wa Yesu Kristo.

Maono Ya Tano: Kinara Cha Taa Cha Dhahabu Pamoja Na Shina La Mafuta (4:1-7)

Shida mbele ya pazia katika maono haya ambayo ilikuwa inachangia hamu dhaifu ya wakimbizi wa Kiyahudi ilikuwa jukumu lao walilopewa na Mungu kushiriki Neno Lake kwa ulimwengu wote, walikuwa na wajibu wa kuishi na lile Neno mbele ya ulimwengu pamoja na

kulishiriki nao. Kifusi cha Hekalu, mji, na taifa lao pamoja na maisha yao wenyewe kiliwafanya kujihisi kwamba walikuwa watu wasiostahili kuwa mfano bora au waalimu wa Neno la Mungu.

Je! Umewahi kuwa katika jangwa la kiroho kupitia magonjwa, uzito wa moyo, au katika aina nyingine ya hali ya kushindwa wakati muovu anapowashilisha mashtaka kinyume chako? Je! Amewahi kukunong'onezea nyakati hizo za uchovu na udhaifu mwingi kwamba *'wewe unahitajika kuwa mfano kwa ulimwengu wote kuona - chumvi ya dunia pamoja na nuru ya ulimwengu?'*

Wakati Zekaria alipofungua ile pazia, alimwona Roho Mtakatifu ambaye aliwakilishwa na yale mashina mawili ya mafuta: *'Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi* ***(*****4:6).'** Maono haya yaliwahakikishia kwamba Mungu atawawezesha kuwa kile Alichokuwa akiwaita kuwa, na kutenda kile alichowaita kutenda, kwa uwezo wa Roho mtakatifu. Hapa ndipo, kama nabii Yoeli, Zekaria anatupatia unabii wakushangaza wa Siku ile ya miujiza ya Pentekoste.

Maono Ya Sita: Chuo Kinachoruka (5:1-4)

Shida iliyotiliwa mkazo mbele ya pazia katika maono haya ilikuwa wakimbizi waliojawa na shida na nguvu za muovu. Wakati nyakati na sehemu ya dunia tunamoishi ni mbaya, ni rahisi, ingawa sio yenye busara, kwetu kujawa nguvu za kutisha za muovu. Udhalimu na ujeuri wa nguvu hizi za kutisha za muovu zilikuwa zikiwahakikishia watu wa Mungu kuwa nguvu za wema na za Mungu hasitawahi kushida nguza za muovu.

Zekaria alipoifungua ile pazia yake ya mawazo tena, aliona nyuma yake, na kuwadhihirisha watu kupitia mahubiri yake, kwamba Bwana wa Majeshi angewahami hili kushinda nguvu za uovu. Kulingana na maono haya ya Zekaria, Mungu ndiye huongoza na kuiweka mipaka, na kwa njia fulani kutumia uovu kwa ajili ya utukufu wake, na kutimiza nia yake. Ingawa hakuna cho chote kizuri kuhusu uovu, Mungu huweka uovu kulingana na mpango wake wa wema pale ambapo watu wake wahusika **(Isaya 45:7; Warumi 8:28).**

Maono Ya Saba: Mwanamke Aketiye Kapuni (5:5-11)

Shida iliyotiwa mkazo na Zekaria mbele ya pazia inayotoka katika maono haya ni udanganyifu au hila kwenye masoko ya ulimwengu. Wakati Zekaria alipofungua ile pazia, alidhihirisha kweli kwamba udanganyifu kwenye masoko ya ulimwengu umewekewa mipaka na Bwana wa Majeshi - na mwishowe kuwekewa vikwazo kutoka Kwake.

Ingawa hatufahamu hayo, kama ilivyo uovu wote uliopo katika uliwengu huu, Mungu hutumia uovu hili kutimiliza malengo Yake na kujitukuza mwenyewe. Kama vile mhunzi wa lulu au mawe ya thamani atumiavyo weusi kudhihirisha urembo wa almasi, Mungu hutumia weusi wa uovu kudhihirisha upendo wake usio na masharti. Upendo ule ulidhihirishwa katika msamaha na ukombozi wa watu Wake kutoka utumwani na pia utadhihirishwa kupitia wokovu ambao tunaweza kumrudia Mungu naye kuturudia.

Maono Ya Nane: Magari Manne Ya Farasi (6:1-8)

Shida ambayo Zekaria aitilia mkazo katika maono haya yalikuwa ni serikali ya kibinadamu ambayo ilikuwa fisadi kiasi kwamba watu wa Mungu walikuwa hawana imani nayo. Kote ulimwenguni siku ya leo, kuna ufisadi mkuu katika serikali za wanadamu, hivi kwamba watu wenye stahi wamepoteza imani kwa mfumo wa kisiasa, pamoja na viongozi wao.

Kile Zekaria alichoona nyuma ya pazia lile ni sawa na ujumbe wa Mika. Mfumo wa serikali ulio bora ni ule wa ufalme wa Mungu. Hadi wakati Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana atakapotawala, hapatakuwa na serikali ambayo haina aina fulani ya ufisadi. Hata hivyo, jinsi ilivyokuwa katika maono mawili yaliyotangulia, Mungu yupo usukani. Mungu wa Majeshi hutenda apendavyo. Serikali ya ufalme wa Mungu itakuwa na mfumo na muundo ulio mtimilifu na wenye utangamano.

Unabii Wa Zekaria Kuhusu Masihi

Wengi wa viongozi wa watu wa Mungu hawakuamini katika Masihi-Mkombozi, na walikuwa vikwazo kwa wale walioamini hivyo. Unabii wa Kimasihi wa Zekaria ulionyehsa kwamba hapo mwisho, Mungu atamwinua na kuweka katika kiti cha enzi Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, ambaye ataunganisha wajibu wa nabii, kuhani na mfalme katika utawala wake wa miaka elfu moja.

Baadhi ya unabii wa Zekaria alitabiri kuja kwa Masihi kwa mara ya mwanza katika mistari hii: **3;8; 9:9, 16; 11:11-13; 12:10; 13:1, 6).** Unabii mwingine kuhusu Masihi na mjio wake wa pili ni katika mistari hii: 6:12; **8:20-23; 14:1-9).** Moja ya mistari hii ni unabii wa Zekaria ambao unaorodhesha kurejeshwa kiroho kwa Wayahudi. Baadhi ya Wasomi wa Biblia huamini kwamba unabii huu unawezekana kuwa ulitimizwa sehemu moja wakati wa Pentekoste ilhali utatimizwa kikamilifu siku za mwisho **(8:20-23).**

Sura Ya Kumi Na Mbili

Unabii Wa Malaki

Katika Nchi ya Marekani Kaskazini, kumezuka viongozi wa kiroho ambao wameanguka katika juhudu zao za kimaadili na kiroho. Kitabu cha mwisho katika Agano la Kale kina ujumbe kwa viongozi wa kiroho. Hosea alifanya maelezo sahihi aliposema kuwa: '*Kama alivyo kuhani, ndivyo walivyo watu* **(Hosea 4:9).**' Hiki ndicho kinachosababisha kuanguka kwa kiongozi wa kiroho kuwa baya sana kwa watu wa Mungu, na kazi na utukufu Wake. Malaki anaonyesha dhihirisho la kuanguka kwa kiongozi wa kiroho. Kusudi lake ni kuwaonyesha wale wanaoongoza watu wa Mungu jinsi ya kuzuia mtindo huo wenye mauti na jinsi ya kurejeshwa kwa uhusiano wao na Mungu wakati wanapoanguka.

Malaki alimfuata Hagai na Zekaria kwa karibu miaka mia moja, na Nehemia kwa takribani miaka kumi. Yeye alikumbwa na shida zile zile ambazo zilimkumba Nehemia, kama kuzuka kwa talaka, zinaa na ukuhani wenye ufisadi **(Nehemia 13:23-25).** Tangu wakati alipoungana na

manabii wengine kuzihesabia zile shida kuwa zinatokana na ukuhani fisadi, anaelekeza ujumbe wake kwa makuhani ambao walikuwa wachungaji wa kiroho wa watu wa Yuda.

Huyu nabii mwenye ujasiri mwingi atatangaza kwamba makuhani walikuwa wameacha njia ya Mungu, na hawakuwa wakimtii bali walifanya watu wengi kutenda dhambi kwa mashauri yao maovu. Tabia ya kuhani ilikuwa yenye aibu mbele ya macho ya watu, na walikuwa wakiuelekeza *'ukuhani kuwa ni mzaha mbaya* **(2:7-9).'**

Alikuwa nabii wakati watu wa Mungu walipokuwa wakienenda katika desturi na mila, huku wakiwa na mfano wa dini uliokataa ukweli wa uhusiano na Mungu. Walikuwa na ubaridi wa kiroho na wenye kukatisha tamaa kiasi kwamba yule nabii mcha Mungu alisononeka. Unabii wa Malaki ulikuwa maonyo kwa viongozi wa kiroho, kwa watu wa Yuda kwamba taratibu na mfumo usio na uhai ungekuwa mojawapo ya njia ya kueleza kiwiliwili kilichokufa.

Nabii huyu wa mwisho katika Agano la Kale hakuhuburi kuhusu maono jinsi Zekaria alivyofanya, au Hagai alivyowapa changa moto watu wa Mungu kulijenga Hekalu. Mzigo wa moyo na ujumbe wake ulikuwa kwamba Mungu alitaka kuwa na uhusiano na watu Wake, lakini makuhani na watu wa Yuda hawakushughulika kumjua na kumpenda Mungu. Sawa na Hosea, Malaki aliamini kwamba watu wa Mungu walikuwa wakifanya usherati wa kiroho na ulimwengu huu.

Wakati Kristo aliyefufuka ambaye anaishi alipoandika barua kwa kizazi cha kwanza cha Kanisa katika mji wa Efeso, aliwakemea kwa kuwa '*Umeuwacha upendo wako wa kwanza* **(Ufunuo 2:4).**' Shida-kikwazo alichozungumzia nabii huyu mcha Mungu ni kwamba watu wa Yuda, hasa makuhani, walikuwa wameacha upendo wao wa kwanza - uhusiano na Mungu - na walikuwa wakiishi maisha ya dhambi.

Anaanza unabii wake kwa maneno haya ya kuvutia: *'Ufunuo wa neno la Bwana kwa Israeli kwa mkono wa Malaki. Nimewapenda ninyi, asema Bwana* **(1:1,2).'** Watu wengi wanapoisoma Biblia, huwa hawatarajii kusoma kuhusu upendo wa Mungu hadi wakati wanapofika katika Agano Jipya, hasa katika mahubiri ya Kristo mlimani. Hawawezi kutarajia kupata dhana ya upendo wa Mungu katika manabii. Upendo wa Mungu kwa hakika, ndio somo kuu katika Maandiko ya manabii kama Maombolezo ya Yeremia, na vitabu vya Hosea, Yona na Malaki.

Kulingana na watu hawa wa Mungu katika Agano la Kale, Mungu aliwapenda kwa upendo ambao hauna kifani na haupatikani kwa matendo mema, au kupotezwa katika matendo mabaya. Mzigo wa unabii wa Malaki ulikuwa kwamba Mungu aliwapenda makuhani na watu wa Yuda. Malaki alipokuwa akishiriki mzigo wa moyoni mwake, aliungana na wale ambao walikuwa wamenukuu na kutangaza kwamba Mungu aliwapenda watu wake kwa vyo vyote bila masharti na alinuia kuwa na uhusiano wa upendo pamoja nao.

Ingawa upendo wa Mungu hauna masharti, kwa kuwa mioyo yao ilikuwa na ubaridi kwake Mungu, na kwamba walikuwa wakiishi katika dhambi, Malaki alihubiri kwamba makuhani na watu wa Yuda walikuwa wakiumiza moyo wa Mungu wa upendo. Mzigo wa Malaki ulikuwa kuonyesha uasi, moyo baridi na ukuhani wenye dhambi kwa watu wa Yuda, jinsi uhusiano wao na Mungu ulivyokuwa umevunjika na jinsi ungerejeshwa. Kusudi kuu la unabii wa Malaki lilikuwa ni ufufuo katika mioyo ya makuhani na wale ambao waliwajibika katika uchungaji.

Mfumo Wa Uandishi Wa Malaki

Malaki alitumia mfumo wa uandishi ambao ulilingana na ule wa Habakuki ulio na busara. Ikiwa umewahi kujaribu kama mzazi kuwasiliana na kijana aliyeasi, kwa hakika utafurahia mfumo huu wa uandishi ambao Malaki alichagua kuwasilisha ujumbe aliopewa na Mungu kwa watu Wake. Sawa na mfumo wa uandishi wa Habakuki, unaweza kutaja mfumo huu wa Malaki kama uandishi wa mjadala au wenye mada au hoja.

Katika unabii wa Malaki, anatoa hoja ambalo yeye anajaribu kuwaambia makuhani na watu wa Yuda jinsi ambavyo wametengana katika uhusiano kati yao na Mungu. Kila wakati anapotenda hivi, watu wa Mungu wanakataa mashtaka yake, na kama ilivyo kwa kijana anapokabiliwa na mzazi, watu wanauliza, *'Ni nani, ni Mimi?'* au, *'Sisi tulitenda hayo wakati gani?'* Nabii anaonyesha kwamba ni Mungu anayesilisha mashtaka haya. Watu nao wanapinga mashtaka hayo yote na kukataa kukubali kweli ya hoja kutoka kwa Baba wa mbinguni kupitia nabii huyo mwaminifu.

Kuna mifano saba kuhusu hoja ya aina hii, ambayo ndio mfumo wa uandishi wa mjadala na pia ndio mwongozo wa kitabu hiki chote. Msomi mmoja wa Biblia aliyenifanya kufunguliwa ufahamu wangu kuhusu manabii, alitaja mifano hii saba ya mjadala kama, 'Manong'onezo Saba Ya Moyo Wenye U Baridi Kwa Mungu.'

SURA YA KUMI NA TATU

Manong'onezo Saba Ya Moyo Wenye Hu Baridi Kwa Mungu

Nong'onezo La Kwanza: Kutilia Shaka Upendo Wa Mungu (1:1-5)

Wakati Malaki anaanza unabii wake kwa tangazo hili: *'Ufunuo wa neno la Bwana kwa Israeli kwa mkono wa Malaki. Nimewapenda ninyi, asema Bwana,' mjadala wa kujibizana kwa maneno: 'je! Haya yalikuwa wakati gani?'* Kwa kuhusika katika mahojiano hayo, huyu nabii anagusia ushahidi mwingi wa upendo wa Mungu kwa watu wa Yuda.

Kila ushirika wa upendo una hatua mbili. Hatua hizo ni kutoa na kupokea upendo. Swali kwa njia isiyodhihirika kabisa lipo hapa. Swali hilo ni hili: *'Ikiwa wewe hauko karibu na Mungu kama ulivyokuwa hapo awali, basi ni nani aliyesonga mbali?* au *'Ikiwa hauna ushirika wa upendo kwa Mungu, lakini hapo awali ulikuwa nao, ni nani aliyeacha kupenda?'* Wakati tunapotilia shaka upendo wa Mungu kwetu, hiyo ni kumaanisha kuwa kuna jambo ambayo sio swa katika upendo wetu kwa Mungu.

Katika kitabu cha Ufunuo, viongozi wale ambao wamekuwa wachungaji wa watu wa Mungu kwa miaka elfu, wanaelezwa kama wazee ishirini ambao wamekaa juu ya viti vidogo vya enzi kuzunguka kiti kikuu huko mbinguni. Wazee hawa wanaelezwa kama waliovaa mavazi meupe, na kuvishwa taji za dhahabu kwenye vichwa vyao. Tunasoma kwamba kila mmoja wao alikuwa na kinubi, bakuli au vitasa vilivyojaa na ubani **(Ufunuo 4:4; 5:8).**

Mavazi hayo meupe ya wazee yaliwakilisha usafi wa maadili, au kwamba wao walikimbia vyema hadi mwisho. Taji zao za dhahabu ziliwakilisha ushindi wao wa kiroho wa imani. Tunaelezwa kwamba bakuli au vile vitasa vilivyojaa ubani vilikuwa maombi ya watu wa Mungu kwao, na kweli kwamba kila mmoja wa wazee hao alikuwa na kinubi, ni dhahiri kwamba walikuwa waabudio.

Kwa kuwa Malaki anaelekeza unabii wa hasa kwa viongozi wa kiroho walio wafisadi, ambao mioyo yao imekuwa na u baridi kwa Mungu, tunaweza kusema kwamba anawaambia kila mmoja wa hawa viongozi wa kiroho kwamba kurudi nyuma kwao katika kuasi kulianza wakati 'Walipopoteza vinubi vyao. ' Yeye alikuwa na mzigo mzito kuhusu matokeo ya kushangaza ya viongozi wa kiroho wanaofanyika baridi katika uhusiano wao na Mungu. Viongozi ambao hawana fursa ya ibada na maombi ya kibinafsi, au wale ambao 'wamepoteza vinubi vyao' hapo baadaye hupoteza yote, kulingana na Malaki.

Ni kwa hali gani ambayo watu wa Mungu huwa wafu kiroho? Kulingana na Malaki, utaratibu huu huanza wakati kiongozi wa kiroho anapotilia shaka upendo wa Mungu kwake mwenyewe, na kupuuza kawaida taratibu yake ya kuabudu na kufanya maombi ya kibinafsi ambayo ni dhihirisho la upendo wao kwa Mungu. Ukweli huu kwa hakika, unapatikana kwa kila mwaminifu wala sio tu kwa kiongozi wa kiroho.

Nong'onezo La Pili: Kulidharau Jina La Mungu (1:6-2:4)

Shtuma lingine la Mungu kupitia Malaki linaeleza nong'onezo la pili ambalo ni moyo wenye u baradi kwa Mungu. Hata hivyo, nong'onezo la pili ni wakati kiongozi wa kiroho au mwaminifu anapolidharau jina la Mungu. Kule kujibizana kunaendelea kwa kukataa, *'ni lini tulilidharau jina la Mungu?'* Jibu lasema kwamba, *'kila mara unaposema, 'usijihusishe kumtolea Mungu cho chote ambacho ni cha thamani kwa Bwana.'*

Malaki anawaambia makuhani hawa: *'Wakati mnapokubali kisha kuwatoa wanyama wagonjwa, vipofu na wenye kulemaa kama dhabihu kwa Mungu, ninyi mwalidharau jina Lake.'* Katika mojawapo ya ujumbe wenye nguvu wa Malaki, akizungumza kwa niaba ya Mungu kwa makuhani hawa, anatangaza hivi: *'Mungu atawapaka mavi nyuso zenu, mavi ya sadaka zenu; nanyi mtaondolewa nayo **(2:3)**.'* Malaki anatangaza kwa sauti kuu: *'Laiti angekuwepo kwenu mtu mmoja wa kuifunga milango;msije mkawasha moto bure madhabahuni pangu!* **(1:10)**.'

Jina la Mungu linawakilisha maana ya Mungu ni Nani na ni Nini? Ukaguzi wa makini wa majina ya Mungu katika Biblia kwa hakika, ni masomo ya asili ya utu na sifa Zake. Sheria ya tatu kati ya hizo kumi inatuonyesha kwamba tusilitaje jina la Mungu bure **(Kutoka 20:7).** Sheria hii haikatazi lugha ya matusi, ila inatuamrisha tusilinene jina la Mungu katika ibada bila kuwa heshima kuu kwa kumtambua Yeye ni nani, na kuitwa kulingana na makusudio Yake. Wakati Yesu aliwafunza mitume wake jinsi ya kuomba, baada ya kuwaambia wamtaje Mungu kama Baba yao aliye mbinguni, Yeye aliwafunza kwamba ombi lao liwe la kwanza, *'Jina lako litukuzwe* **(Mathayo 6:9).'**

Wakati watu wa Yuda walipokuwa wakimtolea Mungu dhabihu hizi duni, na makuhani hao kuzipokea, watu hao waliozitoa walikuwa wakilidharau jina la Mungu. Wao walikuwa wakifanya tangazo kwamba Mungu hakustahili cho chote cha thamani. Utumishi wetu pia unadhihirisha yale tunayofikiria kuhusu Mungu na kile anachostahili kupokea kutoka kwetu. Kulingana na Malaki, nong'onezo la pili la moyo unaofanyika baridi kwa Mungu ni kulidharau jina Lake.

Je! Wewe unajiona mwenyewe katika manong'onezo haya ya moyo? Je! Wewe una fursa ya kibinafsi, na ya kipeke, na ukaribu, na ibada ya kibinafsi pamoja na ushirika na Mungu? Je! Unaonyesha kwa kuabudu kwako kwamba unampenda Mungu na kumpokea jinsi na yale anayostahili?

Nong'onezo La Tatu: Ahadi Iliyovunjika Kwa Mungu (1:13)

Wakati kiongozi wa kiroho, au mwaminifu ambaye hadhihirishi upendo wa kibinafsi na Mungu katika Ibada ya kibinafisi na kipekee, na kuonyesha kwa matendo yake kwamba analidharau asili ya Mungu, nong'onezo lifuatalo katika moyo wake ni kwamba ainaichukulia kuwa ngumu kazi ya Mungu. Malaki kwa njia isiyodhihirika kabisa alieleza swali lingine kwa makuhani. Swali hilo ni hili: 'Je! Umechoshwa na kazi, au hauna hamu ye yote?' Hapa, anawapa makuhani changa moto, hasa wale wenye kunata-nata na kunungíunika kwamba kazi ya Mungu ni ngumu sana kwa swali hili: 'Je! Kazi ya Mungu ni ngumu sana, au je! Umeacha upendo wako wa kwanza na haumpendi Mungu kwa nafsi yako yote?'

Sasa nakukumbusha kwa maneno yale yaliotiliwa mkazo katika unabii wa Hagai ambayo yapatikana katika Biblia: 'Mungu Kwanza!' Kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, tunapewa changa moto kuweka Mungu kwanza na kumwabudu peke yake. Wakati kiongozi wa kiroho anamtumikia Mungu kwa moyo uliogawanyika, haichukui muda mrefu kabla hajagundua kwamba kazi ya Mungu ni ngumu sana. Watu walio na huzuni kuu ulimwenguni ni viongozi wa kiroho, au wale wamchao Mungu, na wanaomtumikia huku wakiwa hawajajitolea kikamilifu.

Tafuta maana ya ukweli huu katika Biblia: *'Ikiwa Mungu ni cho chote kwako, hivyo basi Mungu ni kila kitu kwako. Kwa kuwa, hadi wakati Mungu atakapokuwa kila kitu kwako, hakika hatakuwa kitu kwako.' Mtizame Eliya akiwapa changa moto watu wa Mungu juu ya Mlima Karmeli kwa swali: 'Ni mpaka lini ndipo mtashawishika kuwili?* Ikiwa Bwana ndiye Mungu, basi mfuateni Yeye na ikiwa Baali ndiye Mungu, basi mfuateni yeye.' Pia msikilize Kristo aliye hai anapoliandikia Kanisa la Laodikia barua kuwa: *'Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingelikuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi kwa sababu una uvugu-vugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu* **(Ufunuo 3:15,16).'**

Yakobo anatuambia kwamba ikiwa watu wenye nia mbili ni watu wenye kusita-sita katika njia zao zote. Na kama vile tayari tumetambua, Yesu alifundisha kwamba nia moja au mtazamo mmoja, hutuongoza katika maisha yaliyojaa furaha, ilhali 'nia mbili za kiroho' hutuongoza katika giza kuu, au kutokuwa na furaha **(Mathayo 6:22,23).** Neno la Mungu limejaa Maandiko ambayo yanatuhimiza kumtumikia kwa nia moja.

Asili Ya Kuhani (2:5-9)

Huku akifanya mazingara ambayo kupitia kwake, atawasilisha shtaka la nne katika sura ya pili, Malaki anatupatia maelezo ya ufasaha kuhusu tabia ya kuhani wa Mungu aliye wa kweli jinsi alivyotumainiwa kuwa. Kwa hakika, yeye ananukuu maneno yaliyonenwa na Musa kuhusu Lawi, baba mkuu wa makuhani: 'Sheria ya kweli ilikuwa kinywani mwake, wala udhalimu haukuonekana midomoni mwake; alikwenda pamoja nami katika amani na unyofu, na kuwageuza wengi hata wakaacha uovu **(Malaki 2:6; Kumbukumbu la Torati 33:10)'**

Kama wakfu kwa wachungaji wasio wa kawaida, na wenye kujitolea, ambao wamewatumikia kwa miaka mingi, baadhi ya makusanyiko fulani yamenakili maneno ya Musa na Malaki kwenye bao na kuwekwa mahali ambapo paweza kuonekana na kila mmoja Kanisani kwa ajili ya vizazi vijavyo kusoma.

Maelezo ya Malaki kuhusu kuhani bado yanazidi kutuambia kwamba: kwa maana yapasa midomo ya '*kuhani' ihifadhi maarifa, tena yawapasa watu **7)** kinywani mwake; kwa kuwa yeye ni mjumbe wa Bwana wa Majeshi* **(**Malaki baadaye analinganisha kielelezo cha jinsi kuhani anapaswa kuwa mwenye hu baridi, kafiri na fisadi ambaye ndiye atakayetangaziwa shtuma la nne, pamoja na sehemu kubwa ya unabii huu.

Nong'onezo La Nne: Ahabi Zilizovunjika Za Ndoa (2:10-16)

Punde tu baada ya makuhani na watu wa Yuda walipokubaliana agano zao kwa Mungu Mtakatifu na mkamilifu, jinsi tungetarajia, ni kitambo tu kabla yao kukubaliana katika agano zao na wenzi wao wa ndoa. Hebu jaribu kufuatilia utaratibu wa manongíonezo haya moyo. Wakati agano lako pamoja na Mugnu linapokumbwa na hitilafu, ni kweli kwamba basi agano lako kwa watu huwa kama ganda la mkate - ambalo asili yake ni kuvunjika-vunjika.

Malaki sasa anazungumzia kuhusu shida ya talaka. Yeye anaungana na Nehemia katika kuhusika kwake kwa watoto ambao wamo katika ndoa ambayo huishia mahakamani kwa talaka **(Nehemia 13:23-25).** Yeye anawakumbusha makuhani pamoja na watu wa Yuda, kwamba ndoa ni mpango wa Mungu kuwapa watoto miaka ishirini ya malezi kabla ya kuwaachiia kuishi maisha yao wenyewe. Hii ndiyo sababu Mungu huchukia talaka **(15).**

Sulemani alituambia kwamba wazazi ni kama upinde nao watoto ni kama mishale. Jinsi watoto wanavyoingia katika maisha inategemea msukumo na mwelekeo wanaopokea kutoka kwa wazazi wao. Ikiwa ulikuwa muovu, na ulifahamu kuwa mafumbo ya Sulemani yanawakilisha ukweli kuhusu jinsi watoto wanapewa malezi na kutayarishwa katika maisha yao, basi ungefanya nini? Yamkini labda ungejaribu kuikata kamba iliyo kwenye upinde huo. Hivi ndivyo yule muovu alivyokuwa akitenda wakati nabii huyu wa mwisho alipokuwa akihubiri. Yaonekana kwamba ni dhahiri kuwa yule muovu atenda hivyo katika desturi zetu za leo.

Kumbuka kwamba Malaki anakagua manongíonezo ya moyo yanayofanyika kwa hu baridi kinyume cha Mungu. Yeye anawaonya watu wa Yuda kwamba kujitolea kwao kwa Mungu kumevunjika, na pia kule kujitolea kwao kwa watu kutavunjika hivi karibuni.

Lengo lake kuu ni kuzungumzia viwango ambavyo mioyo ya makuhani imefanyika kuwa baridi kinyume cha Mungu, na kuwaongoza mahali ambapo wanaichukulia talaka kuwa jambo la kawaida kwa kupokea dhabihu za watu walio talakiana. Kwa ufasaha, Malaki anawashtumu watu hawa walio talakiana kwa kufunika madhabahu kwa machozi yao, huku wakilalamika kwamba Mungu ameondoa baraka zake kutoka maishani mwao. Yeye anaendelea kueleza kwamba Mungu ameziondoa baraka zake kwa waume wa Yuda kwa sababu wao wamewafanyia udhalimu wake kwa kuwapa talaka. Wake zao walikuwa waaminifu kwao tangu ujana wao. Wao walikuwa wameiweka nadhiri yao kwa Mungu na wake zao kwamba wataishi nao kwa wema au ubaya, hadi watakapotenganishwa na kifo. Kuivunja nadhiri hii yao kulikuwa ni udhalimu, kulingana na Malaki.

Nong'onezo La Tano: Maadili Yenye Kuwiana (2:17-3:7)

Ili kutibu uchungu wa hukumu ya hatia zao, njia ya pekee ambayo wao wangeishi pamoja na kupoteza uadilifu ilikuwa kufanya aina ya 'maadili yenye kuwiana.' 'Uadilifu wao mpya' au 'uadilifu wenye kuwiana' ulizifariji roho zao ambazo zilivunjika kutokana na hukumu ya hatia zao, na kuwapa Wayahudi hawa wa nia mbili kiwango kipya cha faraja ambayo iliwawezesha kuishi maisha yao yenye thamani na mfumo wa dhambi.

Unapofikiria kuhusu uadilifu kamili wa sheria ya Mungu ambayo ilipeanwa kwa Musa, wazo kuhusu 'uadilifu mpya' au 'uadilifu wenye kuwianaí ni matusi makuu kwa elimu ya thiolojia. Sisi huchukulia dhana kuhusu uadilifu wenye kuwiana, au uadilifu usio na maadili wa nyakati hizi za karne ya ishirini na moja, kama kuibuka kwa uadilifu mpya. Ikiwa unaoma juu ya manabii na kuwaamini, basi unafahamu kwamba karibu wote waliungana na Malaki kulizungumzia jambo hili kuhusu uadilifu wenye kuwiana.

Malaki alishtumu makuhani kwamba wao na watu wa Yuda walikuwa wakisema kwamba uovu ni wema, na kuwa watu waovu humpendeza Bwana, Naye hashughuliki na uadilifu **(2:17).** Ikiwa wewe utatupilia mbali ule mgawanyiko wa sura, basi unaweza kuona kwamba Malaki alitumia aina ya usemi wenye fungu mbili katika kupinga uadilifu weny kuwiana wa wale waliokuwa wakitibu hukumu ya hatia katika njia hii.

Kwanza, Malaki aligusia kuhusu kuja kwake Masihi kwa mara ya Kwanza **(3:1-6)**. Swali la Malaki lilikuwa ni hili, *'Ni nani awezaye kusimama wakati Yeye atakapotokea?' 'Ni nani awezaye kuvumilia kuja kwake?' Wakati ajapo, Masihi atakuwa kama moto ulao na kutakasa chuma; yeye atayasafisha mavazi yaliyo machafu kabisa, yeye atatakasa watumishi wake Mungu, naye atayafanya mambo kuwa sawa katika Mji Mtakatifu **(3:4, 5).** Wakati ajapo, Masihi atahubiri kwamba Mungu habadiliki na kwamba Mungu hujihisi vile vile kuhusu mambo ya uadilifu* **(3;6).**

Sehemu ya pili ya mjadala wa Malaki inaendelea katika sura ya 4 na kutilia mkazo mjio wa pili wa Masihi **(4:1, 2; 3:18).** Malaki alikuwa akihubiri jambo moja kuhusu sheria zisizobadilika za Mungu ambazo zinatiliwa mkazo katika Biblia - kwamba Mungu hushughulika na mambo ya uadilifu na kwa sababu hiyo, sisi huyavuna yale tunayopanda.

Nong'onezo La Sita: Kumwibia Mungu (3:8-12)

Nong'onezo hili linasema kuwa makuhani na watu wa Yuda walikuwa wakimwibia Mungu. Kujibizana kunaendelea huku watu wakijibu hivi, *'Tumekuibia kwa namna gani?* Jibu ni kwamba walimwibia Mungu kila wakati walipokataa kumtolea fungu la kumi.

Neno la Kiebrania la 'fungu la kumi' linamaanisha 'moja kati ya kumi.' Umuhimu wa fungu la kumi ni kwamba lilikuwa ni fungu la kwanza kati ya zile kumi kutoka kwa kila kitu ambacho mcha Mungu alipokea katika maisha. Fungu la kumi lilikuwa ni fursa la mwaminifu kujifunza na pia kupima kiwango ambacho yeye alikuwa akitimiza kanuni ya 'Mungu kwanzaí ambayo inazungumzwa kote katika Biblia. Wakati walipovamia Nchi ya Ahadi, yale yote waliyoteka katika mji wa kwanza yalikuwa ya Mungu. Wao walimpatia Mungu wana wao wa kwanza.

Kando na fungu la kumi, sheria ya Mungu iliwashauri waaminifu kufanya matoleo na dhabihu. Daudi alifafanua dhabihu wakati alipoandika: '*Wala sitamtolea Bwana, Mungu wangu, sadaka za kuteketezwa nisizozigharimia* **(2 Samweli 24:24b).'** Umuhimu wa mtazamo wa Malaki juu ya fungu la kumi ni kwamba sehemu ya kwanza ya kumi kutoka kwa yale yote waliyokuwa nayo na kupokea ilikuwa ni dhahiri kwamba yalikuwa ya Bwana. Hii ni kumaanisha kwamba kukatalia na fungu la kumi kulimaanisha kuwa wao walikuwa wanamwibia Mungu kile kilichokuwa chake.

Itilie maanani hali na mazingira kuhusu nong'onezo hili la sita la moyo wenye hu baridi na mgumu kinyume cha Mungu. Nawe kwa hakika utatambua hila inayoongoza kwa hatua katika kuasi ambako umeelezwa na kunukuliwa na nabii: Dhirisho la ibada ya upendo kwake Mungu halimo tena; matendo yao hayaonyeshi ufahamu na shukrani yao kuhusu ufahamu wa utu na asili ya Mungu, pamoja na kile anachostahili; kujitolea kwa Mungu kumevunjika; uhusiano kati yao na Mungu ambao umeharibika hutangulia hali zingine zilizovunjika kati ya watu; kisha maadili wenye kuwiana katika kutibu upotovu wa stahi au heshima.

Wakati tunaposikiza haya manongíonezo matano ya kwanza, tunaweza kutarajia kutotoa kwa fungu la kumi na matoleo. Kwa kuwa nongíonezo hili la sita huja baadaye katika utaratibu huu, naye nabii anaelekeza ujumbe wake kwa makuhani wafisadi, basi tunaweza kutarajia kwamba anamaanisha kwamba ni makuhani ambao walikuwa wakitumia vibaya matoleo na fungu la kumi.

Nong'onezo la Saba: Kutoamini! (3:13-15)

Kutoamini huku kunadhirishwa wakati Malaki akizungumza kwa ufasaha, kwa niaba ya Mungu, alitaja shutuma la saba kinyume cha makuhani na watu wa Yuda - nao wanamjibu: '*maneno yangu yamekuwa magumu ju yangu, asema Bwana. Lakini ninyi mwasema, Tumesema maneno juu yako kwa namna gani? Mmesema, Kumtumikia Mungu hakuna faida; na, Tumepata faida gani kwa kuyashika maagizo yake, na kwa kwenda kwa huzuni mbele za Bwana wa majeshi? Na sasa twasema ya kwamba wenye kiburi ndio walio heri; naam, watendao uovu ndio wajengwao; naam, wamjaribuo Mungu ndio waponywao, 'Heri ni yule mwenye kutakabari!' Kwa kuwa wale ambao huyatenda maovu wao hufanikiwa, na wale ambao humdhubutu Mungu kuwaadhibu wao wao huwa huru.'*

Ingawa hawa makuhani hawakuwa na imani, na kwa kuwa wao walizaliwa katika ukoo wa ukuhani, wao hatimaye hawaacha ukuhani. Hivyo basi, wao waliendelea kutenda kazi kama makuhani. Na kwa kuwa wajibu mmoja wa makuhani ulikuwa kufundisha Maandiko kwa watu wa Yuda, ni yapi walikuwa wafundishe ikiwa wenyewe hawakuamini Maandiko hayo? Kulingana na Malaki, wao walifundisha kwamba *'heri wale wenye kutakabari!'*

Ikiwa una ufahamu wa Biblia, basi unafahamu jinsi Mungu anachukia kiburi na kutakabari. Kiburi ndiye mama wa dhambi nyingi. Hivyo basi, ni kwa sababu gani ambayo makuhani wangehubiri, 'heri wenye kutakabari?' Malaki anatuambia kwamba hawa makuhani kwa wakati huu walikuwa wameenda kando na imani.

Wakati tunaposikia mahubiri ambayo ni dhahiri kwamba yapingana na Biblia, hatuwezi kukosa kushangaa jinsi tumewasili katika hali hiyo ya kuasi na kutokuamini. Jibu kuu la Malaki ni kwamba haya yote yalianza wakati tuliposikiliza manong'onezo ya mioyo yetu. Inaweza kuchukua miaka mingi kwa haya manong'onezo saba kusikika katika moyo wa mwaminifu au kwa kiongozi wa kiroho.

Ukimweka chura katika sufuria yenye maji yanayochemka, kwa hakika ataruka nje. Lakini ukimweka katika maji baridi na kuongeza joto pole pole, yule chura kwa hakika ataiva kabisa. Mfumo huu wenye hila unaelezwa na Malaki kuwa unafanya vivyo hivyo - pole pole - lakini mwishowe matokeo yake ni ufisadi dhidi ya viongozi wa kiroho, na kuchibuka kwa talaka, maadili yenye kuwiana pamoja na kutoamini.

SURA YA KUMI NA NNE

Maneno Ya Mwisho (Malaki 3:16-4:4)

Kusoma kwa uangalifu Maandiko yaliyonukuliwa hapo juu kutaonyesha kwamba ujumbe wa Malaki ulimalizikia katika sura ya tatu na msitari wa kumi na tano. Sehemu nyingine ya unabii wa Malaki ilikuwa ni kumalizia, ambako kulieleza jinsi watu walikumbana na ujumbe huu mkuu wake, hasa wale waaminifu wenye mioyo migumu na hu baridi ambao walikuwa wameacha uhusiano wao na Mungu, au imani yao au hata waliacha yote.

Kote katika unabii wa Malaki, tumelisikia majibu ya Mungu kwa mazungumzo haya ya makuhani na watu wa Yuda wenye mioyo migumu na hu baridi kinyume cha Mungu. Katika kifungu hiki cha kumalizia tunasikia majibu ya Mungu kwao watu Wake. Wale ambao humcha na kumpenda Bwana, walithibitisha mahubiri haya makuu ya Malaki. Wao walikuwa watu wa Mungu ambao hawakuwa wameacha upendo wa wa kwanza, au kutubu na kurudia upendo wa Bwana kupitia mahubiri ya Malaki.

Tunasoma kuwa: *‘Ndipo wale waliomcha Bwana waliposemezana wao kwa wao. Naye Bwana akasikiliza, akasikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele zake, kwa ajili ya hao waliomcha Bwana, na kulitafakari jina lake.’*

Lengo kuu la Malaki lilikuwa kuurejesha uhusiano aliotaka kati Mungu na watu Wake kupitia ufufuo wa kiroho. Kitabu cha Malaki kinamalizia kwa kutuambia kwamba Malaki alilifikia lengo lake kwa sababu maneno haya ndiyo maelezo ya ufufuo.

Maneno ya kumalizia pia yananaukuu jibu nzuri kutoka kwa Mungu kwa majibu ya makuhani wa kweli pamoja na watu Wake. Malaki anaelezea mjio wa pili wa Kristo wakati jua la haki litachomoza likiwa na uponyaji kwenye mbawa zake kwa waaminifu, lakini hukumu kali kwa wenye hu baridi ambao ndio wenye kutiliwa mkazo mkuu katika unabii wake. Yeye anawaambia kwamba wataona jinsi Mungu huhisi kuhusu maadili yenye kuwiana.

Unabii Wa Kumalizia (4:5,6)

Malaki anamalizia mahubiri yake kwa kutuambia kuhusu kuja kwa nabii kama Eliya ambaye angemtangulia na kumtambulisha Yesu Kristo. Yesu ataeleza wazi kabisa kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa ndiye nabii huyo **(Mathayo 11:7-14).** Ili mtu ye yote asije akadhani kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa Eliya, Yohana alikataa kata uwezekano huo **(Yohana 1:21).**

Malaki angemalizia unabii wake kwa maneno haya, ‘Kuendelea - baada ya miaka mia nne!’ Baada ya miaka mia nne ya kimya, wakati Wayahudi hawakuwa na nabii ye yote wala Neno kutoka kwa Mungu, Yohana Mbatizaji alitokea akihubiri katika roho na nguvu ya Eliya. Makuhani, viongozi wa kiroho, na watu wa Yuda walitumia wakati mwingi wakimsikiliza nabii huyu mkuu kuliko wengine.

Wakati Yesu, mwenyewe, alihubiri, viongozi wale wale walitumia wakati mwingi wakimsikiliza Masihi wao. Wengine walijaribu kumpiga kwa mawe, ilhali wengine walipaza sauti zao wakisema, ‘Tumempata Masihi!í Wao walimwamini, wakamfuata na kufanyika mitume Wake.

Imekuwa furaha kuchunguza Agano la Kale pamoja nawe, nami ninamalizia kwa changa moto mbili kwako: **(1)** Je! Wewe utafanyia nini yale umejifunza? Je! Utampiga kwa mawe Masihi atoke ndani ya maisha yako, au utamfuata? Pili, utaendelea kujifunza kutoka kitabu hiki kitakatifu pamoja nasi huku tunapoanza ukaguzi wetu wa Agano Jipya?